

Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa akijadiliana jambo na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa (kulia) na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Festo Dugange (katikati), Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Zitto ataka Jaji Mkuu, DPP wajiuzulu

**Na Mwandishi Wetu**

MWANGWI wa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kutengeneza taasisi za utoaji haki ikiwamo kuwajibishwa kwa baadhi ya viongozi kwa madai ya kuzitia doa, umezidi kupiga maeneo mbalimbali.

Safari hii, sauti ya mwangwi huo imewafikia Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma na aliyekuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Jaji Biswalo Mganga, ambao Chama cha ACT- Wazalendo kimewataka wajiuzulu kwa kuutia doa mhimili wa mahakama katika utoaji haki na utendaji kazi wao.

Hatua hiyo imekuja siku mbili tu baada ya Rais Samia kuzindua tume ikiongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman, kuangalia jinsi ya uboreshaji wa taasisi za utoaji haki, zikiwamo mahakama na ofisi ya DPP.

Rais alisema katika taasisi hizo, kumekuwa na mmomonyoko mkubwa wa maadili, upendeleo na watu kubambikiwa kesi zikiwamo za uhujumu uchumi. Taasisi zingine ni Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Kutokana na Mahakama na ofisi ya DPP kutajwa, Kiongozi wa ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, jana alitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuwa Jaji Mkuu, Prof, Juma na Jaji Biswalo kuwa wajiuzulu kupisha uchunguzi na kulinda hadhi ya mahakama.

"Januari 31, 2023, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua na kuapisha Tume ya Kupitia Haki Jamii nchini na (kuitaka) kuja na mapendekezo ya mabadiliko ya kufanywa.

Katika hafla hiyo, Rais pia alitoa taarifa kwa umma kuhusu sehemu kubwa ya mabilioni ya fedha yaliyokusanywa kwa mtindo wa 'Plea Bargain' na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP) kutokujulikana yalipo," alisema Zitto katika taarifa hiyo.

Alisema kwa ACT Wazalendo, jambo hilo lilishasemwa kwa kina wakati wa uchambuzi wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambaye alionyesha kuwa fedha zilizokusanywa hazijulikani zilitumikaje. "Taarifa hii ya juzi ya Rais imethibitisha yaliyosemwa na CAG na imetonesha vidonda vya uchungu na maumivu makali ambayo Watanzania walipitishwa kupitia mfumo uliopo sasa wa haki jinai," alisema Zitto.

Kutokana na maelezo hayo ya Rais, Zitto katika taarifa hiyo alisema aliyekuwa msimamizi mkuu wa mhimili wa utoaji haki nchini, Mahakama, ambaye bado ni Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma na aliyekuwa DPP, Jaji Biswalo Mganga, hawana tena sifa za kuendelea kutumikia nyadhifa walizo nazo sasa kisheria.

"ACT Wazalendo tunawataka Jaji Mkuu pamoja na Jaji Biswalo kujiuzulu ili kupisha uchunguzi wa kina wa jambo hili na pia kuusitiri mhimili wa Mahakama ambao, tukitumia lugha ya kiungwana, ulinajisiwa mbele ya macho yao. Ni muhimu waondoke ili kulinda hadhi ya Mahakama," alisisitiza.

**ALICHOSEMA RAIS**

Wakati akizundua tume hiyo jijini Dodoma, Rais alisema katika mhimili wa mahakama na ofisi ya DPP, kulikuwa na mabilioni ya fedha yaliyokuwa yanakusanywa kutoka kwa watu waliokuwa na kesi za uhujumu uchumi ili waachiwe.

Hata hivyo, fedha hizo zilizokuwa zikikusanywa katika ofisi hiyo wakati wa serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati Dk. John Magufuli, hazijulikani zilipo au zilitumikaje, huku kukiwa na taarifa mbalimbali ambazo zimesababisha ukakasi wa suala hilo.

"Nyuma hapa kidogo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kulikuwa kuna ngoma kubwa kidogo inachezwa mpaka kukusanya fedha za wale wa 'plea bargaining'. Zingine zimeonekana na zingine hazionekani.

"Ukifuatilia utaambiwa kuna akaunti China sijui imepeleka fedha zipi. Kayatazameni haya yote. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuna nini hasa kilichoiharibu ofisi hii," alisema Rais Samia.

Jambo hilo pamoja na mengine, yalisababisha ofisi hiyo kunyooshewa kidole na wananchi juu ya utendaji wake, hivyo Rais aliitaka tume ya Jaji Chande, kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu uboreshaji wake wa kiutendaji na kimfumo.

Nipashe ilimtafuta Biswalo kwa njia ya simu majira ya saa 11:04 jioni hadi saa 11:17 jioni ili kupata ufafanuzi wake kuhusiana na kauli hiyo ya Zitto, lakini simu zake ziliita bila kupokelewa. Hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maneno kupitia mtandao wa 'whatsapp' haukujibiwa.


JODAC

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**JODAC PROFESSIONAL LIMITED** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L.P 40780 DAR ES SALAAM** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara Magari tajwa hapo chini siku ya Jumanne tarehe 21/02/2023 na Ijumaa tarehe 24/02/2023 mnada utaanza saa 05:00 asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPARATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam,Mwanza , Arusha na Morogoro

| NA | JINA LA MTEJA | MODEL NA. | NAMBA YA GARI | MAHALI DHAMANA ILIPO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | VICENT CHIMI MASANJA | LP010.2T/52 | T387DPZ | MWANZA |
| 2 | SAMWELI KISAKA MZAVA | LPK2519 | T598DMK | MWANZA |
| 3 | ISAYA LWIDIKO SANGA | LP909BUS | T424DNM | DAR ES SALAAM |
| 4 | JULIUS GAMBA MUGETA | LTP709 | T548DXP | MWANZA |
| 5 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | NOVAS | T666DNL | ARUSHA |
| 6 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | NOVAS | T695DNU | DAR ES SALAAM |
| 7 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | NOVAS | T664DNL | DAR ES SALAAM |
| 8 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | NOVAS | T257DNN | DAR ES SALAAM |
| 9 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | NOVAS | T662DNL | DAR ES SALAAM |
| 10 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | NOVAS | T661DNL | DAR ES SALAAM |
| 11 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | NOVAS | T658DNL | DAR ES SALAAM |
| 12 | SAID ADAM UHAHULA | LP909BUS | T178DWE | MOROGORO |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya bei iliyo afikiwa siku hiyo baada ya nyundo ya dalali kutua na salio la 75% liwe limelipwa ndani ya siku 14 kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya 25%na mnada utarudiwa tena
3. gharama za kuona kukagua ,kuamisha umiliki ni juu ya mnunuzi
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa mali yake ndani ya siku tatu(3) baada ya malipo ya 100% kukamilika vinginevyo gharama za kuhifadhi/kutunza mali hiyo itakuwa juu ya mnunuzi
5. Kwa yoyote atakaye haribu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
6. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwenye ofisi zetu zilizopo Victoria, Abla Appartment & Hotels, Ground Floor au tupigie kwa simu zilizopo hapo juu au wasiliana na **JODAC PROFESSIONAL LIMITED au FIKA ALLIANCE FINANCE CORPARATION LIMITED**


# Wafugaji waua kwa panga na shoka ofisa misitu, mgambo

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

KUNDI la watu zaidi ya 200 wanaodaiwa kuwa wafugaji na wanaoendesha shughuli za kibinadamu kinyume cha sheria kwenye Msitu wa Hifahi ya Kijiji cha Chakulu na Ilunde wilayani Uvinza mkoani Kigoma, limedaiwa kuwavamia maofisa misitu na askari mgambo 18 waliokuwa doria na kuwaua watatu.

Imedaiwa kuwa watu hao waliwashambulia askari hao na ofisa misitu kwa kutumia silaha za jadi, ikiwamo shoka na mapanga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Filemon Makungu amewataja waliouawa kuwa ni Ofisa Misitu wilayani Uvinza, Adam Harenga pamoja na askari mgambo; Ibrahim Seba na Moshi Shaban.

Kamanda huyo aliwaambia waandishi wa habari mjini hapa jana kuwa katika msafara huo, maofisa misitu walikuwa 17.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi baada ya maofisa hao kwenda kwenye msitu huo kufanya doria na kukamata ng'ombe ambao walikuwa wameingizwa baada ya kufanyika oparesheni ya kuwaondoa wafugaji.

Alifafanua baada ya maofisa hao kuchukua hatua hizo, watuhumiwa waliitana na kuwazingira kisha kuanza kuwashambulia, baadhi walifanikiwa kukimbia na watatu walipoteza maisha huku mmoja akijeruhiwa.

Kamanda Makungu alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu 46 kuhusiana na tukio hilo na msako mkali unaendelea kwenye maeneo mbalimbali ili kubaini wahusika na hatua za kisheria zitachukuliwa baada ya uchunguzi kukamilika.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kigoma (Maweni), Dk. Stanley Binagi, akizungumzia hali ya majeruhi Juma Nusura ambaye ni askari mgambo aliyejeruhiwa katika tukio hilo, alisema alipokewa akiwa na majeraha makubwa kichwani, mgongoni na kifuani lakini hali yake inaendelea vizuri baada ya kuanza kupatiwa matibabu.

Majeruhi Juma Nusura alisema watu hao waliwashambulia kwa vitu mbalimbali na kutokana na wingi wao na silaha za jadi, baadhi yao walishindwa kujiokoa.

"Walikuwa wengi sana, nilijaribu kutumia uwezo na mbinu mbalimbali kujiokoa lakini sikuweza kwa sababu nilizingirwa na kila mmoja alikuwa akinipiga mpaka nilipozimia na wao kudhani nimekufa," alisema.

Juma ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Uvinza, alichukuliwa na kupelekwa kwenye Kituo cha Afya Uvinza na baadaye kuhamishiwa Hospitali ya Rufani Maweni ambako alizinduka na anaendelea na matibabu.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, akizungumza baada ya kumtembelea majeruhi huyo anaendelea vizuri, aliwaonya wavamizi wa misitu, akiwataka kuondoka kwenye maeneo hayo.

"Hiki ni kitendo cha kinyama na si cha kistaarabu, serikali ipo makini, tutawasaka popote walipo ili sheria ifuate mkondo wake," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Waziri Mkuu atoa kauli viboko shuleni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amelimbia Bunge kuwa serikali haitafumbia macho wala kukubaliana na adhabu kali kwa wanafunzi, akiagiza utoaji wa adhabu uzingatie Waraka wa Elimu Na. 24 wa Mwaka 2002 huku akikemea wanaopiga picha na kusambaza mitandaoni.

Vilevile, ameahidi serikali itashirikisha wadau kuangalia ushauri wa wabunge waliotaka adhabu ya viboko iondolewe au kupunguzwa.

Akitoa ufafanuzi na mwelekeo wa serikali bungeni jana kuhusu adhabu zinazotolewa shuleni, Majaliwa alisema viboko hutumika kama njia ya kumrudisha mtoto kwenye mstari na serikali iliweka utaratibu maalum wa namna ya kusimamia adhabu hiyo bila kuathiri afya na saikolojia ya mtoto.

"Adhabu itazingatia ukubwa wa kosa, jinsia na afya ya mtoto na isizidi viboko vinne kwa wakati mmoja na mwanafunzi wa kike atapewa adhabu ya viboko mkononi na mwalimu wa kike isipokuwa kama shule haina mwalimu wa kike.

"Adhabu ya viboko itakapotolewa, inapaswa kuorodheshwa kwenye kitabu kilichotengwa na mwalimu mkuu, aweke saini kila adhabu hiyo itakapotolewa, na mwanafunzi akikataa viboko atasimamishwa shule," alisema.

Alibainisha kuwa waraka huo uliotolewa na Wizara ya Elimu umeweka adhabu kwa mwalimu atakayekiuka utaratibu.

"Nisisitize kuwa hatua zitachukuliwa kwa walimu wakuu na walimu watakaokiuka utaratibu uliowekwa, na wazazi na wanafunzi tutimize wajibu wetu," alisema.

Waziri Mkuu alisisitiza kuwa pamoja na matatizo yaliyojitokeza, shule bado ni sehemu salama kwa malezi ya watoto na walimu wameendelea kufanya kazi kwa bidii na kujituma.

"Nitoe wito kwa wazazi katika majukumu yao ya kila siku, watenge muda wa kufuatilia mwenendo na maendeleo ya watoto kuzungumza na watoto," alisema.

Waziri Mkuu pia alikemea tabia ya walimu wanaopiga picha matukio ya aina hiyo na kurusha mitandaoni, akiwataka kuiacha kwa kuwa inajenga chuki kwa walimu na taswira hasi dhidi yao.

"Taarifa zitumwe kwa wahusika ili hatua zichukuliwe hukohuko badala ya kuzua taharuki kwa jamii, lengo si kuficha taarifa bali kuzuia chuki na uhasama ndani ya jamii zetu, si kwa walimu tu, bali pia nyanja nyingine kama afya," alisema.

Alikiri kuna udhaifu katika usimamizi wa adhabu ya viboko shuleni na kuwataka Maofisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kuwakumbusha walimu kuzingatia mwongozo wa utoaji wa adhabu shuleni chini ya kifungu namba 61 cha Sheria ya Elimu.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alitaka watoa taarifa za matukio hayo kwa utaratibu unaotakiwa, walindwe.

# Msamaria apokwa mtoto aliyemlea mwaka mzima

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wamemtaka Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Masumbuko Mtesigwa, kumrejesha Masasi mtoto aliyeokotwa jalalani kisha kuchukuliwa na kupelekwa mkoani Tanga katika mazingira yenye utata.

Viongozi hao wamedai kuwa mtoto huyo aliokotwa jalalani Masasi mwaka jana akiwa na umri wa siku mbili na kulelewa na mkazi wa Kijiji cha Chiunguta, Ziada Daniel na juzi alichukuliwa na moja ya familia kutoka Tanga wakidai ni mtoto wao.

Pia walieleza kuwa familia hiyo walisafiri kutoka Tanga hadi wilayani Masasi kwa ajili ya kumchukua mtoto huyo kwenda kumlea mkoani Tanga.

Walitoa maagizo hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani, wakisema kitendo kilichofanyika cha kumnyang'nya mtoto mama huyo ambaye tangu ameokotwa aliamua kujitolea kumlea hadi anafikisha umri wa mwaka mmoja, hakikubaliki.

Diwani wa Mwena, Nestory Chilumba alisema mama huyo ameonyesha moyo wa mapenzi na mtoto huyo tangu akiwa mchanga.

Alisema wanashangazwa kusikia kuna mama na mume wake wametoka mkoani Tanga hadi Masasi na kumchukua mtoto huyo kinyemela.

Alisema Ziada ametumia gharama kubwa kumlea mtoto huyo ambaye alikabidhiwa na Serikali ya Wilaya ya Masasi kumlea.

"Tunakuagiza mkurugenzi haraka ufanye jitihada za kuhakikisha mtoto huyu anarudi Masasi na anakabidhiwa mama huyu aendelee kumlea. Haiwezikani mtoto ameokotwa Masasi na alishajitokeza wa kumlea halafu anyang'anywe na kupewa mtu kutoka Tanga, tunaka mtoto arudi Masasi haraka," alisema Chilumba.

Diwani wa Viti Maalum, Asina Lipopola alisema: "Sisi madiwani wanawake tumeumia moyo kusikia mtoto huyo amesafirishwa kwenda mkoani Tanga huku mama ambaye awali alibeba majukumu ya kumlea kichanga akiwa bado na mapenzi na mtoto huyo."

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Ibrahimu Chiputula alisema baraza hilo halijaridhishwa na taarifa ya mtoto huyo kupelekwa Tanga na kunyng'anywa mama huyo.

Mama mlezi wa mtoto huyo, Ziada aliiambia Nipashe kuwa alikabidhiwa mtoto huyo kumlea na ustawi wa jamii mwaka jana, muda mfupi baada ya mtoto huyo kuokotwa jalalani.

Alisema anashangaa kuona wanakuja watu kutoka mkoani Tanga na kueleza wamekuja kumchukua mtoto huyo ili wakamlee.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Mtesigwa, alisema amepokea maagizo hayo ya madiwani na atayafikisha kwenye vyombo husika ili yafanyiwe kazi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe na Kozi ya lami kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi ya Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki kumi (10)** 10/04/2023 – 17/06/2023 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |
| 2 | Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)** 14/08/2023 - 09/09/2023 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**
**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

**(a) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:**

Kozi hii, Washiriki watajifunza maada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

**(b) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:**

Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbalimbali juu ya ujenzi wa barabara za lami (Surface Dressing for low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni: Maada juu ya vifaa na Mitambo midogomidogo, Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na matengenezo ya barabara za lami.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe/udongo kwa wiki kumi (10) itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

Kozi ya Lami kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo itaendeshwa kwa muda wa wiki nne (4) ni Kiingereza.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

a) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo
   i. Mshiriki atakaye jitegemea huduma za chakula na malazi, atalipa ada kiasi cha Tsh. 800,000.00; na
   ii. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,600,000.00

b) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads)
   i. Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,000,000.00

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**

**MKUU WA CHUO**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**
**ICoT,**

**S.L.P 963,**
**MOROGORO.**
**Simu** : 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
**Nukushi** : 023-2935227
**Barua pepe** : mwti@morogoro.net

**S.L.P 1957,**
**MBEYA.**
**Simu** : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404
**Nukushi** : 025 295 7486
**Barua pepe** : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

# Waziri Mwigulu, Mpina watunishiana misuli

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SAKATA la mfumuko wa bei limeibuka tena bungeni, safari hii Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina akisema hauwezi kudhibitiwa kama usimamizi wa bajeti hauko sawa kwa kufanya malipo nje ya bajeti.

Mpina alitoa kauli hiyo bungeni jana alipochangia taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Maji na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii huku Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba akipinga kilichoelezwa na mbunge huyo.

Waziri Nchemba aliwaeleza wabunge kuwa wanapotoa taarifa ndani ya Bunge wawe na uhakika nazo na kufafanua kwa kina maeneo ambayo serikali ililazimika kulipa fedha nje ya bajeti.

Mbunge Mpina alisema sababu kubwa za mfumuko wa bei serikali yenyewe kutokana na usimamizi hafifu wa sheria na sera za fedha.

"Huwezi kudhibiti mfumuko wa bei kama unaweza kufanya malipo nje ya bajeti, kama usimamizi wako wa bajeti hauko sawasawa, unaweza kufanya malipo nje ya bajeti Sh. bilioni 350 tumemlipa Symbion fedha ambazo hazipo kwenye bajeti, huwezi kupata utulivu wa fedha.

"Huwezi kupeleka fedha zilizopangwa kwenye maeneo husika lakini pia kuingia mikataba mibovu kama ulioingiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) wa Sh. trilioni 6.34, mkataba wenye shaka wenye malipo zaidi ya trilioni 1.7 halafu ukategemea utapata utulivu wa fedha nchini," alisema.

Waziri Nchemba akijibu hoja hiyo, alisema fedha ambazo mbunge huyo anasema zimelipwa si zilizolipwa.

"Ni vizuri sana waheshimiwa wabunge, tunapoitwa waheshimiwa tunapotoa taarifa kwenye chombo hiki kikubwa, tuwe tunatoa taarifa ambazo tuna uhakika nazo.

"Fedha ambazo tumelipa nje ya bajeti, yapo mafungu kama matatu hivi, tumelipa fedha nje ya bajeti baada ya kugundulika kuna wanafunzi 29,000 wamekosa mikopo ya elimu ya juu, tukaja bungeni tena kwa azimio mkasema tafuteni fedha kokote watoto waende vyuoni, tumekwenda kuchukua Sh. bilioni 86 watoto wetu wapo vyuo vikuu hivi ninavyoongea," alisema.

Alitaja eneo la pili ni la malipo ya Sh. bilioni 160 zilizolipwa kwa ajili ya kujenga madarasa 800 ili mwaka huu watoto waliotakiwa kwenda kidato cha kwanza waripoti shuleni kwa wakati mmoja.

"Anapotokea mbunge na kusema tumetoa fedha nje ya bajeti na kuishambulia serikali kama vile imefanya uamuzi mbaya, nadhani lazima kuwe na kasoro katika kufikiria.

"Kama mzazi huwezi kuchukia wanafunzi maskini kupewa mkopo, nilitamani na nilidhani wabunge makini wangemshukuru Mheshimwa Rais kwa kuchukua uamuzi huo wa kutoa fedha watoto wote wakapata mikopo.


"Haya mambo tusiwe tu tunatamani kushambulia serikali hata kama haijafanya makosa, ikifanya makosa ikosoeni, hizi ndizo fedha zimetoka nje ya bajeti, hizi fedha wala haziwezi kusababisha mfumuko wa bei, sijui ni uchumi wa wapi ukijenga madarasa unasababisha mfumuko wa bei," alisema.

Waziri huyo alisema wanavutia wawekezaji waje kuwekeza ili wakishawekeza watanzania wapate ajira na nchi ipate kodi.

"Kwamba unamhurumia maskini kwa kuzuia uwekezaji, unawasababisha maskini waendelee kuwa maskini, wekeza ili wapate kazi ili watoke kwenye umaskini, wekeza ili wapate ajira ili watoke kwenye umaskini, wekeza ili upate sekta binafsi kubwa ili ilipe kodi ili uwatoe maskini kwenye kulipa kodi.

"Maskini wakibaki peke yao utaendelea kuwatoza wao wenyewe, tunaleta wapya, tunaleta kampuni mpya za uwekezaji tunaleta sekta binafsi ikue ili tuweze kuitoza tuwahurumie maskini.

"Hebu tujadili mambo mengine huko yanayohusu uganga wa kienyeji, kwenye uchumi ni taaluma yangu, mnajadilije vitu bila kufuatilia? Ninataka tusimvunje moyo Mheshimiwa Rais anavyohurumia maskini, anataka sekta iendeshe uchumi wake, leo hii watumishi wa umma ndiyo walipakodi kwa sababu hawawezi kukwepa," alisema.



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa tatu kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh milioni 90 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Lake Gas, tawi la Mwanza, Ali Abeid Salum (wa tatu kulia), jijini Dar es Salaam jana, ambaye kampuni yake ni moja ya kampuni 16 za nishati safi ya kupikia zilizonufaika na ruzuku kutoka Mpango wa Tanzania CookFund unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) ukilenga kusaidia kampuni hizo kutoa huduma kwa bei nafuu na zenye ubora unaowanufaisha wateja wa kipato cha chini katika maeneo ya vijijini na mijini nchini. Wengine ni Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti (katikati), Mkuu wa Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF) Tanzania, Peter Malika (wa pili kulia) na wadau wengine. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA**
**Bidhaa za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT), Elektroniki.**

**REF ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0112**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za awali za ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia Mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa utoaji wa huduma ya Ugavi wa:

**- Vitu vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ununuzi wa vifaa vya kielektroniki**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha. Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA UPEO WA VIFAA / HUDUMA:**
- Ugavi wa vifaa vya elektroniki vya ofisi
- Mashine za kupiga chapa (printer) / kutoa vivuli (copier) / skena au kisoma maandishi (Scanner)
- Vifaa / Vitu vya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT)

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:
- Wasifu wa kampuni na uthibitisho wa rasilimali za kutosha za kifedha na zenye uwezo.
- Uthibitisho wa Cheti au Hati Safi ya Mlipa kodi ya Kampuni
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi husika / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika ugavi na uuzaji wa bidhaa zinazohitajika za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
- ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli za matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, unapendekezwa sana.
- Orodha ya vifaa pamoja na modeli / chapa/ tovuti ya mtandao unaozitangaza/shiti za kiufundi (technical sheets).

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **17 Februari 2023 , 1800hrs** Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA**
**Samani za Ofisi**

**REF ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0111**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za awali za ujenzi wa Gati na kituo cha upakiaji katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

**- Samani za Ofisi**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
- Samani za Ofisini,
- Meza za Ofisi,
- Meza maalumu za Kazi za Ofisi (Work stations)
- Makabati ya Faili ya chuma
- Viti vya Ofisi (Manager chairs)
- Rafu ya vitabu ya mbao/ makabati ya mbao

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:
- Wasifu wa kampuni na uthibitisho wa rasilimali za kutosha za kifedha na zenye uwezo.
- Uthibitisho wa Cheti / Hati safi ya Mlipa kodi ya Kampuni.
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi / rekodi husika inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza kazi zinazofanana na kuuza Samani zinazohitajika kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
- ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli za kuzingatia rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, unapendekezwa zaidi.
- Orodha ya samani zinazouzwa na maelezo ya modeli / chapa / tovuti au mtandao zinakotangazwa / maelezo ya kiufundi (vipimo/aina ya mbao).

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa barua pepe na viambatanishi : 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **17 Februari 2023 , 1800hrs** Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

## HABARI KITAIFA

# Wafurika Muhimbili kuwekewa puto tumboni

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imesema inapokea idadi kubwa ya wananchi kwa siku wanaotaka kuwekewa puto tumboni ili kupunguza uzito.

Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Prof. Mohamed Janabi alibainisha hayo alipohojiwa na moja ya vituo vya redio jijini Dar es Salaam juzi kuhusu huduma ya kuwekewa puto iliyoanzishwa na MNH-Mloganzila.

Alisema baada ya mafanikio makubwa ya uwekaji wa puto ambalo huwekwa bila kufanyiwa upasuaji, watu wengi wamefurahia huduma hiyo na wamekuwa wakijitokeza kupata huduma hiyo.

"Siwezi kutaja idadi ila kwa kweli baada ya kuanza kwa huduma hii, Mloganzila tumepata idadi kubwa ya watu wanaotaka kuwekewa puto na kwa wastani kila siku kuna watu wanawekewa puto," alisema Prof. Janabi.

Alisema puto hilo hupunguza ukubwa wa tumbo na kumsababishia mhusika kula kidogo na kujihisi kushiba, hali ambayo mwisho wa siku inamsababishia kupungua kwa mwili haraka.

"Kinachofanyika ni kuweka puto sehemu ya tumbo na kuweka maji kidogo kuziba nafasi kubwa iliyoko tumboni ndiyo sababu mhusika akila kidogo, anasikia kushiba. Sasa, kwa kuwa chakula ni kidogo lazima mwili utapungua," alisema Prof. Janabi.

Alisema puto hilo huwekwa kwa muda wa miezi minane na baada ya hapo hutolewa na mhusika kupewa elimu ya namna ya kula kwa staha ili asirudi kwenye uzito wake wa awali.

"Tukikuwekea puto lazima utapungua kwa sababu ile nafasi iliyokuwa inabeba chakula haipo. Lakini tukilitoa ukarudia ulaji wa zamani lazima utaongeza uzito ule uliokuwanao awali tunakuwekea puto lingine na utatoa tena Sh. milioni nne," alisema.

Aliongeza kuwa watu ambao wamekuwa wakiwekewa puto ni wenye uzito unaozidi kilo 90, akibainisha kuwa mtu mzito zaidi ambaye wameshamwekea puto la kupunguza uzito, alikuwa na uzito wa kilo 240.

"Chini ya kilo 90 hatukuwekei puto, ukija tutakupa elimu kuhusu namna ya kula na kubadili mtindo wako wa maisha kwa ujumla ili usiendelee kuongeka uzito," alifafanua Prof. Janabi.

Alipoulizwa iwapo aliyewekewa puto anaweza kupata madhara kama atafanya mazoezi mazito, Prof. Janabi alisema puto hilo siyo la kawaida kama yale wanayochezea watoto mitaani.

"Unajua watu wanadhani tunaposema puto ni hili puto ambalo wanachezea watoto mitaani. Hili puto ni maalum na ndiyo sababu linawekwa kwa milioni nne. Kwa hiyo, haliwezi kuharibika kwa mhusika kufanya mazoezi au kufanya shughuli yoyote," alisema.

Prof. Janabi alitoa wito kwa wananchi kujitahidi kuzingatia kanuni za afya kama kula mlo kamili na kufanya mazoezi ili kuepukana na gharama kama hizo za kuwekewa puto tumboni.

Miongoni mwa watu maarufu waliowekewa puto ni msanii Peter Msechu ambaye alisema hivi karibuni kwamba puto hilo limemwezesha kupungua uzito na anafurahia huduma hiyo.

# Katibu Mkuu CCM abaini kikwazo kipya cha miradi

**Na Mary Geofrey,**
MALINYI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amesema kuwapo vigingi vya misamaha ya kodi kwa vifaa na mitambo ya ujenzi wa miradi ya maendeleo ni kiini cha kukwama kwa miradi mingi nchini.

Ameshauri kuwapo kwa dirisha moja litakaloshughulika na misamaha ya vifaa na mitambo ya miradi ya maendeleo inayoingia nchini.

Chongolo aliyasema hayo jana Ifakara wilayani Kilombero mkoani Morogoro alipokuwa anaendelea na ziara ya kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo, uhai wa chama na kusikiliza kero za wananchi.

Alikagua maendeleo ya ujenzi wa daraja la Mto Ruaha Mkuu ambalo ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa barabara kuu ya Mikumi- Kidatu-Ifakara-Mahenge/Lupiro-Malinyi hadi Lumecha yenye urefu wa Km 547 inayounganisha Mkoa wa Morogoro na Ruvuma.

Alibaini mradi huo kuchelewa kuanza kutokana na mlolongo wa misamaha ya kodi kwa vifaa na mitambo ya ujenzi wa miradi ya maendeleo vinavyoingia nchini.

"Serikali ni moja, msamaha wa kodi tunatoa wenyewe, mradi tunasainisha wenyewe, halafu jambo moja la msamaha wa kodi linakuwa nyuma, linachukua muda mrefu wakati wa kutia saini mradi linakuwa mbele, nadhani ifike mwisho wa tatizo hili.

"Kuanzia sasa serikali inapaswa kuweka mfumo wa kuhakikisha msamaha wa kodi hauwi kikwazo tena kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo," alisema.

Alifafanua kuwa msamaha wa kodi maana yake mradi umechakatwa na kukubaliana kuwa utatekelezwa kwa kuondoa kodi, hasa ya Ongezeko la Thamani (VAT).



Nipashe
MWANGA WA JAMII



# Vitendo vinatakiwa zaidi sasa kukomesha utapeli mtandaoni

**KWA** muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kuongezeka kwa wimbi la watu wanaotumia mitandao ya simu za mkononi kufanya utapeli ikiwamo kuibiwa fedha au kutumiwa ujumbe mbalimbali ukiwamo wa vitisho.

Baadhi ya watu hao wanaotumia mitandao, wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali ikiwamo kuwaambia wananchi kwamba wamepokea fedha kimakosa, hivyo wafuate maelekezo wanayopewa ili kurejesha kurejesha miamala inayodaiwa kukosewa. Matokeo yake, baadhi ya watu wameibiwa fedha zao bila kujitambua na wanapofuatilia kwenye kampuni za simu husika, wanaambiwa kuwa miamala hiyo haitambuliki.

Aidha, baadhi ya watumiaji wa simu za mkononi, wamekuwa wakitumiwa ujumbe kwamba watoto wao walioko shule za bweni wanaumwa na wamelazwa hospitalini, hivyo wanatakiwa kutuma fedha kwa ajili ya matibabu. Kutokana na baadhi yao kuamini kwamba inawezekana watoto wao wanaumwa, hulazimika kutuma fedha na wanapokuja kushtuka, wanajikuta wameibiwa fedha zao.

Kwa jumla, kila uchao matapeli hao wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali zinazofanikisha azma zao za kuwaibia wananchi. Miongoni mwa mbinu hizo ni kutakiwa kulipa fedha kwa njia ya simu kwa kutumia namba fulani na kutuma fedha kiasi fulani kama wanavyoelekezwa ili kujiunga na Freemason.

Kama vile haitoshi, watu wameanza kupokea simu kwamba mganga wa kienyeji aliyeko sehemu fulani ni mtaalamu wa kumpa mtu utajiri, dawa ya mvuto kwa mchumba na kadhalika.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo vya utapeli ambavyo vimewaingiza watu wengi mkenge, juzi, Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Nape Nnauye, aliibuka na kusema dawa ya watu hao inachemka na watashughulikiwa wakati wowote.

Waziri Nape ametoa kauli hiyo ikitoa matumaini kwa mara nyingine kwamba sasa watu wanaotumia mitandao kujitajirisha na wakati huo huo kuwaumiza wengine, sasa ujanja wao umejulikana na watakiona cha mtema kuni.

Pamoja na kauli hiyo yenye kutia matumaini, si mara ya kwanza kwa Watanzania kusikia jambo hilo kwa kuwa limekuwa likisemwa mara kwa mara na viongozi wa ngazi mbalimbali waliopewa dhamana ya kusimamia sekta ya mawasiliano. Licha ya kutoa kauli hizo na kwamba mwisho wa watu hao umefika, vitendo hivyo bado vinaendelea kuota mizizi.

Kwa mantiki hiyo, kutokana na hali iliyofikia kwa vitendo hivyo, itoshe kusema kwamba maneno yameshindwa na sasa vitendo vitumike, ikiwa na maana kwamba serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iwachukulie watu hao hatua kwa mujibu wa sheria badala ya kuendelea kutoa kauli tamu ambazo katu hazisaidii.

Tunasema hivyo kwa sababu watu hao namba zao zimesajiliwa kwa mfumo wa kielektroniki, hivyo wanajulikana kwa majina yao na namba zao za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Kwa mantiki hiyo, ni rahisi kuwapata na kuwachukulia hatua kama nia thabiti ya kufanya hivyo itakuwapo.

Ni dhahiri kwamba kama TCRA, na kampuni zinazotoa huduma za simu za mkononi na jeshi la Polisi watashirikiana kwa dhati, jambo hilo linaweza kufanyiwa kazi na kukomeshwa mara moja. Ni muda wa vitendo sasa maneno yawekwe kando.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Serikali, wazazi tuumize kichwa chanzo 'madenti' kufeli hisabati

**KWANZA** kabla ya yote, niseme tu kuwa somo la hisabati halijawahi kuwa rahisi popote pale duniani, achilia mbali Tanzania.

Ni somo ambalo mwanafunzi yeyote anayelimudu vema, anatazamwa si tu shuleni na familia, hata na jamii kama si mtu wa kawaida anakuwa wa kuheshimika.

Kuna baadhi ya wanafunzi hawapendi kuliona wala kulisikia. Wanaamini ni somo linalowasumbua ubongo tu, kwani kwenye maisha hawaendi kukutana nalo, japo ukweli wanajidanganya.

Wanaamini safari yao ya maisha wanaenda kukutana na mambo mengine tu, kama kuajiriwa na kufanya kazi, biashara, mapenzi, mambo ya kijamii na yanayofanana na hayo.

Wanaamini somo la hesabu linawafaa wanafunzi watakaoenda kufanya kazi za fedha, urubani, ukandarasi na zinazohitaji zaidi mahesabu, kuliko masomo mengine.

Kitu ambacho wengi hawaelewi ni kwamba, kwa binadamu, chochote anachofanya ni mahesabu. Kuanzia anapoamka asubuhi, anapotembea hadi anaporudi tena nyumbani kulala.

Kupanda kulala saa sita na kutakiwa kuamka saa 11:00 alfajiri ni hesabu tosha. Kuamka asubuhi, kupanga muda wa kunywa chai, hadi kufika ofisini kwa muda unaotakiwa, pia ni mahesabu.

Barabara inabidi uvuke kwa mahesabu, hata ukiangalia jengo lilivyojengwa, nazo ni kwa hesabu kali.

Nijumuishe, muundo wa maghorofa, nyumba tunazoishi, vyoo, vifaa vya teknolojia, nazo ni zao la hisabati na vimetengenezwa kwa mahesabu.

Nitoe mfano mdogo tu, mvua zikinyesha, maji huwa hayatuami pale barabarani na inapokuwa imejengwa kwa mahesabu bora, athari hazitokuwapo.

Ni kwamba hujengwa ikiwa upande mmoja umeinama na mmoja umeinuka, maji ya mvua yatatiririka kwenda upande mmoja.

Hesabu zingine kwa watengenezaji ni kwamba, baadhi ya barabara kati kuna mgongo, yaani pameinuka, halafu kwenda kushoto na kulia kunakuwa na mteremko ili kufanya maji kutiririka pande zote.

Kwa macho ya kawaida, inatajwa ni ngumu kuliona hilo. Hata wanaojenga vyooni, hufanya hivyo ili maji yanayomwagika pande zote yaende kwenye shimo.

Hapa nimetoa mfano wa vitu hai tunavyoishi navyo, kuhusu mahesabu. Mjenzi wa nyumba ana kitu kinaitwa 'pima maji'. Ni kifaa cha kimahesabu kinachomuongoza mjenzi asipindishe ukuta.

Kwa maana hiyo hesabu hazikimbiwi sehemu yoyote kwenye maisha. Hata bajeti ya nyumba, nini kinunuliwe kwanza cha umuhimu na nini kisubiri ni hesabu zinatumika.

Pamoja na kwamba hesabu si somo pendwa, lakini kwa miaka ya karibuni watahiniwa wameonekana kufanya vibaya zaidi, tofauti na zamani. Hapa kuna tatizo lazima lifanyiwe kazi haraka sana.

Kuna sehemu wazazi na serikali lazima wakae chini, ikiwamo kuwashirikisha wataalamu, ili kuangalia tatizo liliko.

Mwishoni mwa wiki Baraza la Mitihani (NECTA) lilitangaza matokeo ya mitihani ya kidato cha nne. Pamoja na kwamba ufaulu umeongezeka, lakini kwa somo la hesabu umeshuka na hali ni mbaya.

Takwimu walizotupa, kati ya watahiniwa 520,558 wa somo hilo, 415,844 hawakufaulu, hivyo kuwa na asilimia 79.92 ya wanafunzi ambao hawakufanya vema kwenye somo hilo.

Najua hakuna kitu chochote kinachotolewa kama fasheni tu au kuonyesha jinsi gani wanafunzi walivyofeli. Ila NECTA hesabu hapa wamemaliza kazi yao na hesabu hizi zimetolewa ili wanaohusika wafanye kazi zao.

Tukianza kwa serikali, yenyewe ina wataalam wengi, hivyo sasa wasikae maofisini tu, waanze kuzunguka na kufanya utafiti kwanini 'madenti' wanaonekana kufeli somo hilo kila kukicha, halafu waje na majibu kama uwezo mdogo wa walimu wa eneo hilo au kuna mengine zaidi?

Kwa wazazi, mimi ni mmoja kati yao. Naweza kuainisha baadhi, nikianza na ukweli kwamba, siku hizi wazazi wanawalea watoto 'kimayai' sana, kiasi kwamba wanashindwa kukabiliana na changamoto za kutenda na kufikiri.

Malezi ya wazazi zamani yalionekana kuwatesa watoto au kuwapa baadhi ya mambo wayafanye wenyewe; kufua nguo, kupika na kazi nyingi nyumbani, kwenda sehemu ya umbali mrefu, na mengine yanayofanana na hayo yaliwafanya wawe na uwezo mkubwa wa kufikiri na kutenda.

Hesabu zinamtaka mtoto mtulivu, mwenye uwezo wa kufikiri na kutenda kwa haraka. Mtoto yeyote ambaye hapati changamoto hata nyumbani, hesabu kwake lazima ziwe ngumu.

Nadhani wazazi tuanzie hapo. Tusiwadekeze sana watoto wetu kiasi kwamba wakikutana na changamoto ndogo tu ya kutumia akili, au kutenda inakuwa tatizo.

# Chongolo awaagiza ma-DC kuwasweka ndani watendaji

**Na Mary Geofrey,** MALINYI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amewaagiza wakuu wa wilaya kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo kuwaweka ndani watendaji na wenyeviti wa vijiji ambao wamekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi nchini.

Chongolo alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na wananchi nyumbani kwa mjumbe wa shina namba tano kwenye Kijiji cha Itete wilayani Malinyi mkoani Morogoro.

Katibu Mkuu yupo katika ziara ya siku tisa kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo, uhai wa chama pamoja na kusikiliza na kuzitatua kero za wananchi.

Chongolo alisema migogoro mingi ya wakulima na wafugaji inasababishwa na wafugaji kutoheshimu ardhi ya wakulima na kunakosababishwa na watendaji na wenyeviti wa vijiji wasio waadilifu.

Alisema wafugaji wakipitisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima, lazima kuna kiongozi aliyewasaliti wananchi hao na kuruhusu wapite.

"Wakuu wa wilaya simamieni sheria, chukueni hatua madhubuti bila kumwonea mtu. Ukibaini kuna mtendaji aliyeruhusu mifugo ikaingia kijijini, kamata sweka ndani, itaweka nidhamu na kudhibiti kukithiri kwa matukio haya ambayo imekuwa kero kubwa nchini," aliagiza Chongolo.

Awali Katibu wa Shina hilo, Geofrey Mgobore, akiwasilisha kero hiyo kwa niaba ya wananchi wa Malinyi, alisema migogoro mingi inatokana na wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na wanapohoji wanapigwa.

Alisema hata wanapokwenda kushtaki kwa viongozi wa halmashauri ambao ndiyo wenye mamlaka ya kuuza maeneo, wanawajibu 'tatizo lenu ni umaskini'.

Chongolo aliwahakikishia wananchi hao kuwa Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Sebastian Waryuba atafuatilia na kutafutia ufumbuzi wa kina wa tatizo hilo.

Alimtaka Waryuba kutumia elimu yake ya sheria na nafasi yake kutafuta ufumbuzi wa kina wa tatizo hilo kwa kushuka chini kujiridhisha na taaarifa zinazotolewa na wananchi hao.

Mkazi wa Kijiji cha Mtimbila, Jane Masine alitaja kero nyingine ni kutozwa gharama kubwa za maji hata kama hawajatumia huduma hiyo.

"Katibu Mkuu hapa tuna shida ya kuletewa bili ya gharama kubwa za maji, hata kama hujafungua bomba la maji gharama za malipo ni kubwa kuanzia 5,000 kwa mwezi, jamba ambalo siyo sawa," alisema Masine.

Akijibu kero hiyo, Chongolo alitoa wiki mbili kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na mkuu wa wilaya hiyo kufanya utafiti wa kina wa jambo hilo na kutafuta suluhu ya kudumu ili wananchi wapate huduma kwa bei stahiki.

Katika hatua nyingine, Chongolo aliwahakikishia wananchi wa Malinyi kuwa serikali imetenga Sh. bilioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa barabara Ifakara-Malinyi, Lupilo hadi Namtumbo mkoani Ruvuma yenye urefu wa Kilometa 396 na ujenzi wake utaanza baada ya upembuzi yakinifu kukamilika.

# Sifuri inavyoitesa shule ya wenye mahitaji maalum

**Na Restuta James**

TATIZO la wanafunzi kupata sifuri katika sekondari ya viziwi Njombe, halijapatiwa tiba licha ya kufikishwa bungeni miaka minne iliyopita.

Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne uliofanyika mwaka jana yaliyotangazwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), yanaonyesha kuwa wanafunzi wote wa Sekondari ya Viziwi Njombe wamepata wastani wa F, yaani sifuri.

Matokeo hayo yanaonyesha kuwa waliofanya mtihani huo shuleni hapo walikuwa wanafunzi 25 na kati yao 23 wamepata daraja sifuri wakati wawili wamepata daraja la nne.

Wanafunzi wawili ambao wamepata daraja la nne mmoja amepata D mbili za Jiografia na Kiswahili na mwingine amepata D tatu za Uraia, Historia na Kiingereza pamoja na C ya Kiswahili.

Hata hivyo, wastani wa shule kwa mujibu wa NECTA ni F.

Matokeo ya wahitimu 21 waliofanya mtihani shuleni hapo mwaka 2017 yaliyotangazwa na NECTA Januari 2018, yalionyesha kwamba walipata daraja la sifuri jambo ambalo lililazimisha serikali kuingilia kati.

Aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Joseph Kakunda, alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Njombe kufanya uchunguzi kubaini kiini cha matokeo hayo mabaya.

Pamoja na agizo la Kakunda, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, aliitisha orodha ya walimu waliosoma elimu maalumu ili wapatiwe ajira.

Hata hivyo, matokeo ya shule hiyo yaliyotangazwa 2020 yalionyesha kwamba wahitimu walikuwa 33 ambao 17 kati yao walipata daraja sifuri, 14 daraja la nne, mmoja daraja la tatu na mmoja daraja la kwanza. Wastani wa shule ukiwa ni F.

Mwaka uliofuata, wahitimu walikuwa 23; ambao 12 kati yao walipata sifuri, tisa walipata daraja la nne na wawili walipata daraja la pili.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUWASILISHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI HUDUMA ZA UTHAMINI KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMB NA – REQ-00000094**

Kampuni ya EACOP inazialika kampuni zenye uzoefu na sifa kuwasilisha maombi ya nia ya kutoa huduma za uthamini katika Mradi wa **Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).**

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litalofukiwa ardhini, linalokatisha mipaka ya nchi mbili ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika Masoko ya Kimataifa. Bomba litaanzia eneo la Kabaale Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, hadi eneo la Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**

Utwaaji wa kudumu wa ardhi inayohitajika na Mradi wa EACOP unaelekea kukamilika. Wakati wa kipindi cha ujenzi, Wakandarasi wa Ujenzi watahitaji ardhi ya ziada ili kuitumia kwa muda kufanya kazi mbalimbali kando kando mwa mkuza wote wa Bomba la Mafuta. Hivyo, kampuni ya EACOP itahitaji kufanya makubaliano ya kutumika ardhi kwa muda ikihusisha vipande vya ardhi zaidi ya 250, vinavyokadiriwa kuwa na ukubwa wa kati ya ekari 0.5 hadi 1.25.

Kampuni ya EACOP inatafuta kampuni yenye uzoefu wa kutosha ili kuwezesha mchakato wa kupatikana ardhi ya muda itakayotumika kufanyia kazi kwa muda kando kando ya mkuza wa Bomba la Mafuta au kwa shughuli nyingine zozote za maandalizi ya Ujenzi.

**Mawanda ya huduma yatahusisha;**

- Kuthibitisha mahitaji ya ardhi ya muda na Timu za Ardhi na Uhandisi za EACOP katika kila eneo husika
- Kuzingatia matakwa ya ardhi ya muda kama yanavyoelezwa kwa kina katika Mpango wa Usimamizi wa Ardhi wa EACOP
- Kubainisha ardhi na wamiliki wake na kuwashirikisha kuhusu uhitaji wa kutumia ardhi hizo kwa muda
- Kufanya tathmini ya hali ya ardhi kabla na baada ya kutumia ardhi hiyo kwa muda.
- Kufanya makubaliano na wamiliki wa ardhi na watumiaji ili kutumika ardhi hizo kwa muda

**VIGEZO MUHIMU:**

Kampuni zinazowasilisha nia zinapaswa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo::

- Uthibitisho wa Usajili kama Kampuni ya Uthamini toka Bodi ya Usajili wa Wathamini.
- Uthibitisho wa Usajili wa Wathamini wa Kampuni hiyo ya Uthamini toka Bodi ya Usajili wa Wathamini.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu wa kutoa huduma za uthamini chini ya sheria za Tanzania na Viwango vya Fedha Kimataifa kwenye miradi mikubwa nchini Tanzania na maeneo ya vijijini
- Leseni ya biashara.
- Uthibitisho wa Usajili toka Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) au ushahidi thabiti wa maombi ya usajili wakati wa uwasilishaji wa maombi ya nia hii iliyotangazwa.
- Kufuata/kukubaliana na kanuni za Wazawa za Mambo ya Petroli za Tanzania.
- Wasifu wa watendaji watakaohusika katika Mradi ikiwa ni Pamoja na nakala za vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma inayohitajika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni Pamoja na kuwakilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka mfumo wa usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na viwango vya ndani na vya ki-sekta vinayotumika kwa kazi hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi ma Haki za Binadamu.

Kampuni zenye nia uwezo na rasilimali ya kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma maombi ya nia yaliyoandaliwa kwa lugha ya Kiingereza pamoja na nyaraka zilizobainishwa hapo juu kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com (ukubwa usiozidi MB20) kabla au si zaidi ya saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe Jumatano 15 Februari 2023"** Kichwa cha cha barua pepe kiwe: [REQ-00000094] _ Kutoa huduma za uthamini katika Mradi wa EACOP.

Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu**: EACOP itapitia na kuchambua nyaraka ziizotumwa na makampuni yalioonesha nia kulingana na EOI hii, na kisha kufanya tathmini kulighana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila kutoa sababu kwa kampuni husika

# Wapandishwa kizimbani kwa mashtaka ya uhujumu uchumi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WATU watatu wakazi wa Kijiji cha Ukumbi, Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora wamefikishwa kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Tabora wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi.

Hata hivyo, kesi hiyo ambayo ipo kwa Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Tabora, Gabriel Ngaeje iliahirishwa hadi Februari 13, 2023.

Siku hiyo imepangwa kwa ajili ya kupokea ushahidi wa askari wa wanyamapori ambaye aliwakamata watuhumiwa hao wakiwa na vielelezo mbalimbali.

Wakili wa Serikali, Robert Mwambalulu akiwasomea mashtaka watuhumiwa hao alisema walikamatwa na askari wa wanyamapori kwa makosa ya kukutwa na bunduki aina ya gobole, nyara za serikali ikiwamo sikio la nyati na palalala. Mwambalulu aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Mussa Omary Msuya (33), Juma Nasoro (27) na Mussa Gasper (54), na kwamba wote walikamatwa Aprili 19, mwaka jana katika Kijiji cha Ukumbi Siganga wilayani Kaliua mkoani Tabora.

Wakili huyo alisema watuhumiwa hao walikamatwa usiku na askari wa wanyamapori katika maeneo tofauti wilayani Kaliua.

Watuhumiwa wote walikana makosa yao na walierudishwa rumande hadi Februari 2023 ,wataporudishwa mahakamani kwa ajili ya kuendelea na ushahidi wa askari wa wanyamapori aliyewakamata.

Wakati huohuo mkazi wa Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, Lucas Luchembele (40), amefikishwa mahakamani kwa kosa la kukutwa na vyuma 29 vya madaraja mali ya Shirika la Reli Nchini (TRC) vyenye thamani ya Sh. 400,000. Akisoma mashitaka mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mkoa wa Tabora, Gabriel Ngaeje, Wakili wa Serikali, Robert Mwambalulu alisema mtuhumiwa alitenda kosa hilo, Juni 16, mwaka jana katika maeneo ya reli mpya.

Akitoa ushahidi mahakamani hapo, mkaguzi wa reli katika maeneo ya Kata ya Usinge Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, Longino Kalumbu alisema, Juni 17, 2022, alipigiwa simu na Mtendaji wa Kijiji, Martin Sungu majira ya saa 7 mchana kwamba anahitajika katika kituo cha polisi.

Mkaguzi huyo aliiambia mahakama hiyo kwamba aliitikia wito huo na alipofika polisi alitakiwa kuvitambua vyuma hivyo kama ni mali ya TRC.

Aidha, Longino aliendelea kuiambia mahakama hiyo kuwa mtuhumiwa hakumtambua bali aliweza kuviona vyuma hivyo vya madaraja vikiwa vimekatwa vipande 29 kama mali ya TRC.

Kesi hiyo iliahirisha hadi Februari 13,mwaka huu kutokana na kuwa ushahidi wa polisi haujakamilika.




Meneja wa Bia ya Pilsner inayozalishwa na kampuni ya Serengeti (SBL), Wankyo Marando (kulia) na Mwakilishi kutoka Bodi ya michezo ya kubahatisha ya Tanzania, Salim Mgufi, akionyesha kwa waandishi wa habari zawadi zitakazoshindaniwa na wateja wa kinywaji hicho, kupitia promosheni ya "Kapu la Wana" iliyozinduliwa, jijini Dar es Salaam jana, mahususi kwa ajili ya wateja wa Kanda ya Ziwa, Kaskazini na Kusini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamlilia Rais kusota mahabusu miaka mingi

**Na Jenifer Gilla**

NDUGU wa mahabusu waliokaa gerezani kwa miaka tisa kwa tuhuma za ugaidi bila kesi zao kusikilizwa, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan aingilie kati ili wapate haki zao.

Wamesema tangu watuhumiwa hao akiwamo mzee wa miaka 96 kukamatwa mwaka 2013, 2016 na 2017, wamesota gerezani bila kesi zao kupelekwa mahakamani kinyume cha haki za binadamu.

Mmoja wa ndugu wa mahabusu hao, Habiba Hussein, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii.

Alisema katika watuhumiwa hao kulikuwa na watoto wa miaka 15 na 17 ambao wamekosa haki zao za msingi, ikiwamo elimu kutokana na kukaa gerezani muda mrefu kwa madai kuwa upelelezi dhidi yao bado haujakamilika.

Hussein alisema na baadhi ya ndugu zao ni wazee ambao wanaohitaji kuhudumiwa na watu wa karibu na kwamba kukaa kwao gerezani bila uhakika wa kesi zao kusikilizwa kunaathiri afya zao kimwili na akili.

Kwa mujibu wa Hussein, wamekuwa wakifuatilia kesi za ndugu zao kwa miaka tisa sasa bila mafanikio huku wakiamini kuwa ndugu zao hawana hatia.

"Wamepoteza heshima zao kwa kupewa tuhuma chafu za ugaidi wakati mpaka sasa ushahidi wa wapi na upi ugaidi waliofanya hakuna. Familia zao zimesambaratika, watoto na wake zao wamekosa baadhi ya haki zao za msingi," alisema.

Hussein alisema familia inamwomba Rais Samia Suluhu aingilie kati kwa kuwa wanaamini kusomwa kwa kesi ni haki ya msingi ya kila Mtanzania anayetuhumiwa, hivyo hawaoni sababu ya ndugu zao kukaa muda mrefu bila kupandishwa mahakamani.

"Ndugu zetu wananyimwa haki za msingi ambazo serikali ina wajibu wa kumtendea kila raia bila ubaguzi, ikiwamo uhuru wa kujitetea mahakamani mara tu baada ya kukamatwa na kufikishwa mbele ya mamlaka hiyo," alisema.

Alitaja idadi ya mahabusu hao kuwa ni 117 wako katika magereza ya Ukonga na Segerea Dar es Salaam, 23 Maweni (Tanga), 23 Kisonge, Arusha na 21 Gereza Kuu Morogoro, huku wengine wakiwa Mtwara, Butimba, Mwanza na Tabora.

Naye Miki Mkanda ambaye baba yake ni mtuhumiwa, alisema anamwomba Rais awasaidie kesi za watuhumiwa hao zisomwe kwa kuwa hali ya baba yake imedhoofika kutokana na kupata maradhi ya kuambukizwa kikiwamo kifua kikuu.

"Tunamwomba atusaidie hili jambo kwa sababu yeye ndiye mwenye kulitatua. Ngazi zote za kisheria tumezifuata na bado tunaendelea kuzifuata japokuwa tunazungushwa sana lakini hatukati tamaa kwa sababu tunaamini ndugu zetu hawana hatia," alisema.

Naye Zubeda Shabani, mwenye mtoto anayetuhumiwa kwa kesi hiyo alisema wameshakwenda hadi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) jijini Dodoma ambaye alionyeshwa wa kushangazwa na baadhi ya kesi.

"Mfano kesi hii ya Temeke, walitoka wawili wakabaki watatu lakini hawapelekwi mahakamani. Tulipokwenda kwa Mkurugenzi wa Mashtaka akasema hii kesi haipo. Kuwapigia Temeke wakasema ipo tunaifanyia kazi, lakini mpaka sasa kimya," alisema Shabani.

# Wajivunia kupenya orodha waajiri bora

**Na John Badi**

MKURUGENZI wa Rasilimali Watu wa Kampuni ya Huawei Tanzania, Wang Yue amesema anajivunia kutajwa kuwa miongoni mwa waajiri bora nchini na hivyo kuthibitisha hadhi yao ya ubora kiutendaji na usimamizi.

Taasisi ya Waajiri Bora imeiorodhesha kampuni hiyo ya teknolojia ya kimataifa kutoka China kama mojawapo ya waajiri bora wanaozingatia viwango vya kimataifa.

Mpango wa Taasisi ya Waajiri Bora huidhinisha mashirika kulingana na ushiriki na matokeo ya utafiti wao wa mbinu bora za waajiri katika kuhudumia wafanyakazi.

Utafiti huo unahusisha maeneo sita kwenye nyanja ya rasilimali watu yenye mada 20 ikiwamo mkakati wa wafanyakazi, mazingira ya kazini, upataji wa vipaji, mafunzo, utofauti, usawa na ujumuisho, ustawi na vingine kadhaa.

Mpango wa Taasisi ya Waajiri Bora umeidhinisha na kutambua waajiri bora 2053 katika nchi na maeneo 121 katika mabara matano.

"Utambuzi huo ni ushuhuda mwingine wa thamani tunayowapa wafanyakazi wetu, dhamira yetu ya kuweka mazingira bora ya kazi kwa watu wetu.

"Thamani ya wafanyakazi ni muhimu kwani ndio rasilimali yetu kuu na chanzo cha hadithi yetu ya mafanikio. Kupanda kwa ofisi yetu ya Tanzania katika orodha ya Waajiri 20 Bora Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ni jambo muhimu sana na la kujipongeza.

"Tuzo hii inapaswa kuwafanya wafanyakazi wetu Tanzania wajivunie kwani wanafanya kazi kwa Mwajiri Bora anayetambulika barani Afrika. Wafanyakazi wetu ni wa thamani kubwa na sera na taratibu zetu zimeundwa ili kuwasaidia wafanyakazi wetu kukua, kufurahia mazingira wanayofanyia kazi na zaidi ya yote kuwapa motisha ya kuwa bora kila siku inayopita," alisema.

Akizungumzia mafanikio hayo, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Huawei Kusini mwa Afrika, Yu Chen alisema kampuni hiyo inajivunia kuwa na idadi kubwa ya ofisi kwenye ukanda huo.

"Tunajivunia kuona maboresho katika ukadiriaji wetu wa afya ya wafanyakazi, ambayo ni kutokana na programu zetu za afya ya kimwili na kiakili ya wafanyakazi," alisema Chen.

Chen aliahidi kampuni itaendelea kujenga sifa yake kama mwajiri bora, akisisitiza watatilia mkazo zaidi kujenga ujuzi wa TEHAMA. Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Waajiri Bora, David Plink anasema: "Nyakati za kipekee huleta ubora kwa watu na mashirika. Na tumeshuhudia hili katika mpango wetu wa vyeti vya waajiri bora mwaka huu. Waajiri hawa wameonyesha kila mara kwamba wanajali maendeleo na ustawi wa watu wao.

"Kwa kufanya hivyo, kwa pamoja wanatajirisha ulimwengu wa kazi. Tunajivunia kutangaza na kusherehekea orodha ya mwaka huu ya waajiri wakuu wanaolenga watu, Waajiri Bora 2023."



# Wawili jela miaka 20 kwa kukutwa na meno ya tembo

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

WAKAZI wawili wa Kijiji cha Endagire, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, wamehukumiwa kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka 20 gerezani kila mmoja, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukutwa na meno ya tembo bila kuwa na kibali cha uwindaji.

Waliohukumiwa kifungo hicho na Mahakama ya Wilaya hiyo ni John Lulu (42) na Zebedayo Safari (34).

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, alisema washtakiwa hao wametiwa hatiani kwa kosa la kumiliki kinyume cha sheria, meno mawili ya tembo, ambayo ni nyara za serikali.

Hakimu Kimario alisema washtakiwa hao walitenda kosa hilo, Oktoba 23 mwaka 2022 wakiwa katika Kijiji cha Burukeli, Wilaya ya Babati.

Katika hukumu hiyo alisema washtakiwa hao walikamatwa wakiwa wanasafirisha vipande viwili vya meno ya tembo, yenye thamani ya Sh.milioni 35.1 ambayo ni sawa na tembo mzima.

"Baada ya kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka, uliowasilisha vielelezo tisa ambavyo viliithibitishia mahakama kuwa washtakiwa walikutwa na nyara za serikali na kisha kuusikiliza upande wa utetezi, nimejiridhisha pasipo shaka kwamba walitenda kosa hilo.

"Kutokana na kosa hilo mahakama hii inawatia hatiani kwa kuikuka kifungu cha 86 (1) (2) (b) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 ya Sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022."

Kabla ya kusomwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Rusticus Mahundi, akisaidiwa na Wakili Abood Komanya, alidai mahakamani humo kuwa washtakiwa hawana rekodi ya kufanya makosa ya uhalifu ila kwa kuwa wanyamapori wana mchango mkubwa katika pato la taifa, ni vyema mahakama hiyo ikawapa adhabu wanayostahili.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere (katikati) akizindua mikataba ya miradi ya maji Mjini Babati juzi. Aliyeshikilia makabrasha ni mfanyakazi wa Wakala wa maji safi na usafi wa mazingira vijijini (RUWASA) Magreth Joseph. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC awaonya wakuu wa idara matumizi mabaya ya fedha

**Na Steven William,** MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Juma Irando, ameanza kazi kwa mkwara, baada ya kuwaonya wakuu wa idara kwamba atakayetumia vibaya fedha za serikali kwenye miradi hatakuwa salama.

Irando, alionya kuhusu matumizi mabaya ya fedha za umma, baada ya kukabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, Halima Bulembo, aliyehamishiwa Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam. "Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan), analeta fedha nyingi za miradi katika idara mbalimbali za halmashauri yetu. Niwadokeze tu kwamba mimi sio mtu wa kufumba macho. Kwenye hilo, Mkuu wa Idara, ambaye atashindwa kusimamia matumizi mazuri ya fedha hizo, atakiona cha moto na wala huu si moto wa kifuu.

"Nimekuja Muheza, kumsaidia kazi Rais. Kama kuna mtumishi yeyote atachezea fedha za serikali, ni bora aache mara moja maana zitamtokea puani." Mbali na onyo hilo, Irando, aliwaomba viongozi mbalimbali pamoja na wananchi wa wilaya hiyo, kumpa ushirikiano katika utendaji kazi wake. Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo, alisema anakabidhi wilaya hiyo, ikiwa salama na haina kashkashi.

# Mil.840/- zatengwa ufadhili ujenzi wa miradi mipya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA la AKO Tanzania Community Support limetenga zaidi ya Sh. milioni 840 kwa ajili ya ufadhili wa ujenzi wa miradi mipya na uboreshaji wa miundombinu ya sekta ya elimu katika Wilaya za Hai na Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Miradi mipya miwili itakayotekelezwa katika Wilaya ya Hai, itaigharimu Sh. milioni 250, wakati miradi itakayotekelezwa eneo la Moshi Vijijini, inagharimu Sh. milioni 590 na hivyo kufanya miradi yote kuligharimu shirika hilo kuwa Sh. milioni 840.

Jana, Mkurugenzi wa Shirika hilo, Hilda Kimathi, alisema katika Wilaya ya Hai, miradi mipya ya ujenzi inaihusisha Shule Jumuishi ya Wenye Ulemavu, inayojengwa Shule ya Msingi Kibaoni, kwa gharama ya Sh. milioni 100 na Shule ya Msingi Darajani, kunakotekelezwa mradi wa ujenzi vyumba viwili vya madarasa, choo cha wanafunzi na walimu na ofisi ya walimu, kwa gharama ya Sh.milioni 150.

Wakati mradi wa ujenzi wa jiko la kisasa, vyumba vya madarasa na ofisi za walimu katika Shule ya Msingi Uchau iliyoko Moshi Vijijini, utaigharimu Sh. milioni 240.

"Miongoni mwa sababu ambazo zimetusukuma AKO Tanzania Community Support, kujitosa kutekeleza miradi hii ya elimu ni pamoja na uchakavu wa miundombinu na kukosekana kwa kwa miundombinu rafiki katika shule zetu. Jambo ambalo tunaona limekuwa likichangia kushuka kwa kwa kiwango cha elimu nchini.

"Shule nyingi za serikali zinatishiwa na uchakavu wa miundombinu yake, ndio maana tumeamua kuweka mkono wetu kuinga mkono serikali na kuwatua mzigo wa kuchangia gharama za ukarabati wananchi wa maeneo hayo yatakayonufaika."


Miradi mingine ambayo inatekelezwa na AKO Tanzania Community Support katika eneo la Moshi Vijijini ni ukarabati wa shule tatu chakavu za msingi, zilizokuwa zikihatarisha maisha ya wanafunzi na walimu kutokana na vyumba vya madarasa kukatika nyufa na kuharibika vibaya miundombinu yake.

Miradi hiyo pia inaigharimu AKO Tanzania Community Support, Sh. milioni 350, inazihusisha Shule ya Msingi Sungu, Shule ya Msingi Kibosho na Shule ya Msingi Singachini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, AKO Tanzania Community Support, inatekeleza mradi wa ukarabati wa Shule ya Msingi Sungu (Sh. milioni 100), Shule ya Msingi Kibosho (Sh. milioni 50) na Shule ya Msingi Singachini (Sh. milioni 200).

Akizungumzia miradi hiyo, namna inavyowasaidia kurejesha hamasa ya ongezeko la ufaulu, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Uchau, Agness Mbwambo alisema: "Tumepata mradi kutoka Shirika la AKO Tanzania Community Support, wametujengea jiko la kupikia chakula cha wanafunzi na walimu. Kabla ya mradi huu, chakula kilikuwa kikipikwa katika vyumba vya madarasa."

Aidha, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Hans Simmer, alisema AKO Tanzania Community Support, imejikita kusaidiana na jamii, kukarabati shule za msingi ambazo hali ya majengo yake ni mbaya ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Adaiwa kumng'oa jicho mwenzake wakigombea soksi

**Elizabert Seleman,**
SENGEREMA

MWANAFUNZI wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Tunyenye iliyopo Kijiji cha Tunyenye wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Yulitha Seleman anadaiwa kupigwa hadi kung'olewa jicho na mwenzake wakiwa shambani.

Akizungumzia tukio hilo mwanafunzi huyo alisema wakati wanalima katika shamba la shule mwanafunzi mwenzake alichukua soksi zake na kwamba wakati anajaribu kuzichukua ndipo alipopigwa kwa kutumia kiatu sehemu ya jicho na kusababisha kutoka.

Yulitha alisema baada ya jicho lake kutoka mwalimu aliyekuwa naye shambani alimbeba na kumpeleka katika Kituo cha Afya Tunyenye kwa ajili ya kupatiwa huduma.

Akizungumzia tukio hilo baba mzazi wa mtoto aliyeng'olewa jicho, Seleman Nyanda alisema anasikitika kuona mwanaye ametolewa jicho wakati alizaliwa mzima.

Aidha, aliomba serikali kuingilia kati suala hilo ili mtoto huyo aweze kupatiwa matibabu haraka ili aendelee na masomo yake kwani kwa sasa hasomi kutokana na tatizo la jicho hilo.

Baadhi ya ndugu na wananchi wa kijiji hicho, walisema wamelipokea kwa masikitiko tukio hilo na kuwaomba walimu kuwa makini kuwasimamia watoto wanapokuwa katika shughuli za kilimo ili kuepuka kuhatarisha usalama wa maisha yao.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Tunyenye, alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo hakuwa tayari kuelezea.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Kituo cha Afya cha Sengerema, Consolatha Magaka alisema kitendo cha mwanafunzi kumpiga mwenzie ni ukatili wa watoto.

Alisema kufuatia tukio hilo wazazi wanatakiwa kuwajibika pande zote mbili ili mwanafunzi huyo apate matibabu ili aendelee na masomo yake kama ilivyokuwa awali na kuahidi kufuatilia suala hilo.

# Jaji akerwa tabia ya 'kutunishiana misuli'

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, Athumani Matuma amewashauri wananchi kuacha tabia ya kutunishiana misuli mahakamani kwa kesi ambazo zinaweza kutatuliwa kwa njia ya usuluhishi na kuleta amani.

Amesema utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi una tija kwa sababu utapunguza chuki, kuokoa muda wa kufanya shughuli za maendeleo na kukuza uchumi endelevu.

Alitoa ushauri huo juzi kwenye kilele cha maadhimisho ya wiki ya sheria nchini mkoani Shinyanga yaliyofanyika katika viwanja vya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, yakiwa na kauli mbiu isemayo 'Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu wajibu wa mahakama na wadau'.

Alisema mawakili wa serikali na wakujitegemea wanapaswa wawe wanawasaidia wananchi kutatua migogoro yao kwanza kwa njia ya usuluhishi na ile ambayo itashindikana ndipo ipelekwe mahakamani kuliko kuwaacha wakitunishiana misuli kwa kesi ambayo inaweza kuisha kwa usuluhishi.

"Mawakili wa serikali na kujitegemea wasaidieni wananchi kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi, ili kuokoa muda wakatekeleze shughuli za kiuchumi, kujenga udugu, migogoro inaleta uadui na chuki, msiwaache watunishiane misuli mahakamani kesi nyingine zinaisha kwa suluhu," alisema Jaji Matuma.

Katika hatua nyingine alisema Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, imefanikiwa kumaliza msongamano wa mashauri kutokana na kujiwekea malengo ya kufanya kazi, huku akisisitiza kesi kumalizwa kwa njia ya ushuluhishi ili kupunguza au kumaliza mashauri mahakamani.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili wa Kujitegemea Mkoa wa Shinyanga na Simiyu, Shaban Mvungi, aliwasihi mawakili wa serikali na kujitegemea kuongeza kasi ya kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi na kwamba inakwamisha maendeleo na kuongeza uadui katika jamii.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Moses Chilla, alisema serikali mkoani humo imejitahidi kuweka madawati ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, hususani kwenye migogoro ya ardhi na mirathi ili k uhakikisha jamii inaishi kwa amani na upendo.



Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Terry Strong (kushoto) akifuatilia wakati Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa kampuni hiyo, Dk. Kiva Mvungi akitoa ufafanuzi kwa wahitimu wa vyuo vikuu wanaopewa mafunzo maalum na GGML mjini Geita juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu vyuo vikuu kupewa mafunzo GGML

**Na Mwandishi Wetu**

WAHITIMU 50 wa vyuo vikuu nchini wamepata fursa ya kupata mafunzo yanayotolewa na Kampuni ya Geita Gold Mining Ltd (GGML) katika fani mbalimbali ndani ya idara za kampuni hiyo mwaka huu kwa lengo la kuwawezesha kupata uzoefu na kuwa na sifa za kuajirika kwenye soko la ajira.

Akizungumza mjini Geita juzi wakati wa hafla ya kuwakaribisha wahitimu hao waliogawanywa kwenye idara mbalimbali za kampuni hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Terry Strong alisema kuwa kupitia Mpango wa Mafunzo Kazini, kampuni hiyo imekuwa mdau mkubwa katika kuunga mkono mipango ya serikali ya kuimarisha uwezo wa wahitimu kuajiriwa baada ya kutekeleza mafunzo ya kazi na programu nyingine za wahitimu kwa miaka kadhaa.

GGML pia inachangia katika kukuza ujuzi nchini kwa kuwapa wahitimu fursa ya kupata uzoefu wa kazi katika nyanja mbalimbali ya ujuzi.

Mpango wa mafunzo kazini hutoa fursa kwa wahitimu wasio na ajira kupata uzoefu wa kazi ambao utakamilisha masomo yao na kuwapa uzoefu ambao unawasaidia kukubalika katika soko la ajira.

"Programu ya mafunzo hayo inatekelezwa kwa kipindi cha miezi 12 na mwaka huu GGML imetoa nafasi za mafunzo kwa wahitimu 50. Kati yao, wanawake ni 30 na wanaume ni 20. Tungependa kuwatakia kila la heri wanaporipoti leo (juzi) kwa idara zao tofauti," alisema.

Dk. Kiva Mvungi, Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa GGML, liwapongeza wahitimu waliojiunga na GGML mwaka huu na kuwataka kuwa makini na matapeli wa ajira.

"Jihadharini na matapeli! GGML haipokei fedha ili upate kazi au fursa nyingine yoyote ndani ya kampuni. Iwapo utaombwa fedha ili upate ofa ya kazi au unashuku jambo kama hilo, tafadhari ripoti hili mara moja kwa Idara yetu ya Usalama, Kitengo cha Upelelezi," alisema.

Dk. Mvungi aliongeza kuwa tangu GGML ianzishwe, imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na mamlaka za serikali za mitaa kusaidia miradi kadhaa ya jamii katika Mkoa wa Geita kupitia ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na programu za Kitaifa.

"Novemba mwaka jana, GGML ilitambuliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kama mlipakodi anayekidhi viwango vya ubora katika tasnia ya madini nchini na mwezi uliofuata, ilinyakua tuzo mbili katika Tuzo za Chama cha Waajiri Tanzania (ATE); nafasi ya kwanza katika utekelezaji Sera ya Wajibu wa Kampuni kwa Jamii na mshindi wa pili kwenye kipengele cha Mwaajiri Bora wa Sekta Binafsi," alisema.



Ukurasa 12

Rais Samia alivyotoa darasa ughaibuni safari mapinduzi kilimo nchini, sekta inavyoendelea




Ukurasa 13

Mikutano ya hadhara ruksa, ila pa kufanyia kitendawili!


# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 3, 2023

Nipashe




Ukurasa 14

**Darasa la UTT AMIS kwa wote pa 'kutokea' kupitia uwekezaji**

SOPHIA MWAKAGENDA

# Mbunge wa kike mwenye rekodi ya makubwa kuwapigania kinamama

- Anoa mabinti mamia, tuzo tatu za kimataifa
- Ashikia 'bango' bei chai hadi 'kikaeleweka'

**Na Mwandishi Wetu**

SOPHIA Mwakagenda, ni jina kubwa sana kisiasa nchini. Pia, unapomtaja kwenye ulingo wa jinsia yake ya kike, nako si haba, yuko juu zaidi.

Leo hii, huyo ni mbunge kupitia viti maalum kwa tiketi ya CHADEMA, akiwa na wenzake 18, ambao sasa wana kesi kuhusu ubunge wao.

Lakini katika sura ya pili, ana lake jingine, hajifichi akiwa katika sura pana ya unaharakati, kazama katika wajibu wa kupenda kuwatetea kinamama wenzake, staili yake akianika anayoyataka kwa matendo.

Hatua aliyofikia inabeba sura ya mafanikio, hata nje ya siasa, ingawa kuna hoja kwamba ni vigumu kutofautisha ulingo wa siasa na maisha ya kawaida.

Rekodi aliyo nayo ni kwamba ameshafanikiwa kuyainua makundi mbalimbali ya kinamama, wakiwamo wakulima, wanawake na wasichana kwa njia mbalimbali, ndani na nje ya mkoa wa Mbeya, anakotoka.

Akizungumza na Nipashe, Sophia anasimulia kwamba maisha yake kwa muda mrefu, amekuwa akitumikia kusaidia kinamama wa tabaka la chini na uzoefu huo ndio ukamuwezesha kuanzisha taasisi iitwayo 'She Can Foundation' mahsusi kusaidia watoto wa kike.

Anasema hao ni wale mahsusi wanaoishi kwenye mazingira magumu mkoani Mbeya. Anfafanua namna anavyowapata wasichana hao, ni kupitia watendaji wa vijiji na vitongoji, ambao ndiyo wanaofahamu changamoto zao huko waliko.



Mbunge Sophia Mwakagenda. **PICHA: MAKTABA.**

Katika kundi hilo, anawataja ni waliopata mimba za utotoni na kushindwa kuendelea na masomo, pamoja na wanaotoka kwenye familia duni, wote anasema wanakusanywa na kufunzwa utengenezaji nguo za batiki, kushona na kutengeneza viungo mbalimbali vya vyakula.

Mpaka sasa, anasema kuna jumla ya wasichana 500 waliohitimu mafunzo kwenye taasisi hiyo na wameshaanza kujiajiri wakipunguza umasikini.

Sophia anaeleza kuwa, kwa sasa kuna jumla ya wasichana 210 wanaendelea na mafunzo hayo, huku lengo lake kubwa ni kukweza hadhi taasisi hiyo kuwa Chuo cha Ufundi Stadi (Veta), kwa kupanua kozi na kuongeza vijana wa kiume anaowagundua nao wana uhitaji wa namna hiyo.

**ATWAA TUZO**

Kutokana na anayofanya, kabla na baada ya kujitosa kwenye siasa, Sophia anasema imemuwezsha atunukiwe tuzo mbalimbali za kimataifa, kati ya mwaka 2015 na 2020.

Anasimulia kwa hatua kwamba, moja aliipata kutoka taasisi anayoitaja kwa jina 'Arabic Islamic Bank' akisema inatokea Uarabuni. Kimsingi, ni benki yenye matawi mengi katika nchi za kiarabu, ikiwa na makao makuu jijini Amaan, Jordan.

Benki hiyo ikamtaja, Sophia kuwa'Mwanamke Bora aliyesaidia wanawake wa tabaka la chini kwa miaka 10.'

Wengine waliopata tuzo hiyo ni Benki ya NBC pamoja na Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro.

Tuzo ya pili ilihusu 'mwanamke bora aliyesaidia jamii." Hiyo ilitolewa na taasisi iitwayo World Woman Economic Forum ya Uingereza na alipokelea nchini India, kwenye kilele cha mkutano wake.

Sophia anaitaja ya tatu, ni iliyotolewa na taasisi ya Community Leadership Award (CODA) ya Canada. Hiyo, ilihusu mwanamke aliyefanya kazi ya kutoa elimu kuhusu mimba za utotoni katika halmashauri za Chalinze mkoani Pwani, Longido mkoani Manyara na Mchinga Tanga.

**KILIMO BUNGENI**

Upande wa kilimo, Mbunge Sophia, ambaye pia ni mzawa wa Tukuyu wilayani Rungwe, ana historia ya kushikia 'bango' bei ndogo ya zao la chai kwa wananchi wa wilayani Rungwe na matunda yakaonekana.

Ilikuwa baada ya kilio hicho cha mbunge, mtendaji mkuu wa shughuli za serikali bungeni,

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

# Rais Samia alivyotoa darasa ughaibuni safari mapinduzi kilimo nchini, sekta inavyoendelea

## •Ateta na wazalisha mbolea waje kuwekeza

**Na Mwandishi Wetu**

NI hatua sasa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anavuma kimataifa, mikutano mikubwa kila mara anakuwa ni miongini mwa 'wazito' mezani.

Mnamo Januari 25 hadi 27 wiki iliyopita, alikuwa jijini Dakar Senegal, kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi Kujenga Uwezo wa Nchi za Afrika Kujitosheleza kwa Chakula. Kaulimbiu ilikuwa "Kuilisha Afrika: Kujitegemea na Uhimilifu katika Uzalishaji wa Chakula."

Ni safari aliyoambatana na mawaziri wake wanaowajibika na mada hiyo; Hussein Bashe (Kilimo), Dk. Mwigulu Nchemba (Fedha na Mipango) na Saada Mkuya (Waziri wa Nchi Ofisi Rais - Fedha na Uchumi Zanzibar).

Watendaji wengine ni Gerald Mweli (Naibu Katibu Mkuu - Kilimo), Amina Shaaban (Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango -Fedha za Nje) na Wakurugenzi wa Wizara ya Kilimo; Fedha na Mipango na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Ni mkutano uliohudhuriwa na wakuu wa nchi 34 za Afrika, mawaziri wenye dhamana ya kilimo na fedha, magavana wa benki kuu, viongozi wa jumuiya za kikanda (AU, SADC, ECOWAS, COMESA, EAC), pia wabia wa maendeleo, wakuu wa mashirika ya kimataifa, viongozi wa taasisi za sekta binafsi, pia wataalamu kilimo kutoka sekta ya umma na binafsi.

Katika yaliyofanyika yalijumuisha, Rais Dk. Samia, ambaye katika siku za karibuni ameibuka kinara kushiriki na kuongoza mikutano ya kimataifa, jijini Dakar, nako akawa sehemu ya jopo la wakuu wa serikali hizo 34 kueleza masuala muhimu yanayoleta mageuzi ya kilimo, akiwa na mada ya Tanzania na Afrika kwa ujumla.

"Alielezea umuhimu wa kuwashirikisha vijana katika kilimo kwa kutatua changamoto za upatikanaji wa ardhi, mitaji, teknolojia na upatikanaji wa masoko," inaeleza taarifa ya Ikulu na inafafanua:

"Kundi la vijana ni kubwa kwa kutoa mfano kwa Tanzania kuwa ni asilimia 34.5 ya idadi ya Watanzania Milioni 61.7 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022."

Katika hilo, Dk. Samia akatoa elimu kwa viongozi wenzake kwa namna serikali anayoiongoza, inavyoshirikiana na taasisi za fedha kuwezesha upatikanaji wa mitaji, hatua iliyofanikisha kupunguza riba ya mikopo ya sekta ya kilimo kutoka asilimia 15 hadi tisa.

Ni hoja iliyoanika anacholenga kushirikisha vijana katika kilimo kwa kutatua changamoto za upatikanaji ardhi, mitaji, teknolojia na masoko.

Rais Samia, anasema hadi sasa, Dira ya Kilimo ya Tanzania ina ajenda anayoitaja '10/30' inayolenga kuitanua sekta ya kilimo kwa asilimia 10 zaidi ifikapo mwaka 2030.

Anaendelea: "Serikali imeanzisha Programu ya 'Building a Better Tomorrow' (BBT), ambayo itawagawia vijana wa kiume na wanawake maeneo ya hadi ekari 10 kwa kila mtu, yakijumuisha wawekezaji katika mashamba makubwa yenye ukubwa wa kati ya ekari 1,000 hadi 20,000.

"Wawekezaji hao watawezesha vijana kutumia teknolojia bora na kununua mazao yatakayozalishwa kwenye mashamba ya vijana na kuongeza thamani."



Rais Samia Suluhu Hassan, katika kikao na wadau wa kilimo alipokuwa jijini Dakar, Senegal.

**UCHUMI KILIMO UNAVYOENDA**

Wiki hii wakati vikao vya kisiasa vikiendelea nchini, mmoja wao akaibuka akinyooshea hali ya mfumuko wa bei na hasa kwenye vyakula, akiinyooshea kidole serikali kwa kiasi kikubwa, imekuwa ikitumia jibu la vita vya Russia na Ukraine, kuwa sababu kuu.

Hata hivyo, akiwa jijini Dakar Senegal, katika uwasilisho wake wa kina Tanzania inakosimama katika uchumi kilimo na mzizi wa changamoto za sasa, Rais Samia alitolea ufafanuzi wenye mawanda mapana , inayonukuliwa na ripoti ya Ikulu:

"Dunia inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa chakula. Changamoto hiyo inatokana na hali halisi ya ongezeko la watu, mabadiliko ya tabianchi, majanga yaliyoikumba dunia ikiwemo ugonjwa wa UVIKO 19 na vita kati ya nchi ya Urusi na Ukraine.

"Majanga hayo yamesababisha baadhi ya pembejeo za kilimo hususan mbolea kuzalishwa kwa kiwango kidogo na ongezeko la gharama za usafirishaji, hivyo kuathiri upatikanaji na uwezo wa wakulima kumudu gharama hizo.

"Mfumko wa bei unaotokana na bei za vyakula, umesababishwa na hatua za Tanzania kufungua masoko mapya ya mazao ya kilimo iliyovutia wanunuzi wengi wa mazao kutoka nchi jirani na hivyo bei za vyakula kwa walaji wa kawaida kuonekana kuwa zimepanda."

Kwa mujibu wa Rais Samia, kilimo kimekuwa kikikua kwa wastani wa asilimia nne na kuchangia katika pato la taifa kwa wastani wa asilimia 26.9; asilimia 65 ya malighafi za viwanda, asilimia 30 ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi na utoshelevu wa chakula kwa asilimia 100.

"Tumeanza kuchukua hatua za kuongeza bajeti ya kilimo kutoka Dola za Marekani milioni 127.8 mwaka 2021/2022 hadi Dola za Marekani Milioni 414.7 mwaka 2022/2023, kuweka unafuu kwa wawekezaji na wafanyabiashara kupitia sera za kodi, udhibiti (regulatory issues), kuendelea kusimamia amani na usalama wa nchi na vivutio vya uwekezaji," anasema Rais Dk. Samia.

**KAMPUNI ZA MBOLEA ZAJA**

Rais Dk. Samia, akiwa jijini Dakar, Senegal akakutana na kampuni za kuzalisha mbolea kwa kikoa cha kando ya mkutano, katika siku ya kwanza ya kikao hicho cha siku tatu.

Akiwa na uongozi wa OCP Group, kampuni ya kimataifa wazalishaji wakuu wa madini ya fosforasi na mbolea duniani, yenye makao Makuu yake jijini Casablanca, Morocco alitambua na kupongeza mchango wao tangu kuwapo kwao nchini mwaka 2017, katika upimaji wa afya ya udongo, usambazaji na uuzaji mbolea.

Pia, Rais Dk.Samia, akatoa ufafanuzi wa matumizi ya mbolea bado ni madogo, ikiwa ni wastani wa kilo 19 kwa hekta, ikilinganishwa na viwango vya kimataifa vinavyolenga walau kilo 50 kwa hekta.

Katika kikoa hicho na wazalisha mbolea, Rais amewataka kujenga uwezo wa ndani Tanzania kuzalisha na kujitosheleza kwa mbolea, kwa kuanzisha kiwanda cha mbolea, chokaa na jasi (gypsum) kwa ajili ya soko la Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Awali akaiambia kampuni ya OCP kuwa, mfumo wa ruzuku ulioanza kutekelezwa kwenye bajeti iliyoko, umefanyiwa maboresho mengi, ikiwamo kuwa na mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wakulima.

Pia, akakutana na uongozi wa kampuni ya kuzalisha mbole, Yara International ya Norway, ambao wakamweleza Rais Samia, Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kufaidika na mpango wake wa kuboresha afya ya udongo unaotekelezwa na kampuni yao.

"Upimaji wa afya ya udongo utafanyika baada ya kufikia makubaliano yao na Benki ya Dunia na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO)," inaeleza taarifa ya Ikulu.

Kampuni hiyo ikamueleza Rais azma yao ya kuanzisha kiwanda cha mbolea chenye uwezo wa kuzalisha tani 300,000.

Kampuni hiyo ikatangaza azma yake kushirikiana na serikali katika kutekeleza Programu ya kilimo ya BBT, kupitia mfumo wa ushirikiano wa sekta binafsi na ya umma katika kuendeleza kilimo, kwa kuwawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati.

**VIPAUMBELE KILIMO**

Akijadili katika vipaumbele vya kilimo kitaifa aliyojadili na wabia wa maendeleo ya kilimo wakati wa Mkutano wa Pili wa Kilimo na Chakula nchini Senegal, Rais Samia akataja vipaumbele vya uwekezaji nchini ni kwenye mazao ya ngano, mafuta ya kula (alizeti), mazao ya bustani (parachichi) na ufugaji wa nyama na maziwa.

Anasema, asilimia 65 ya ardhi inayofaa kwa kilimo duniani haijatumika na kwa upande wa Tanzania ni takriban asilimia 24 ya ardhi inayofaa kwa kilimo haijatumika.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika picha ya pamoja na Rais wa Senegal, Macky Sally na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Dk. Adesina Akinumwi, kabla ya kuanza kwa mkutano wa kilimo na chakula, Dakar nchini Senegal, Januari 25, mwaka huu. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

TAFAKURI YA MLALAHOI




## Mikutano ya hadhara ruksa, ila pa kufanyia kitendawili!



**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**(kulangwasos@gmail.com)**

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza rasmi kuondolewa zuio la mikutano ya hadhara ya siasa na sasa kuanza kufanyika, kuna changamoto mpya inajitokeza ikihitaji ufumbuzi.

Ni jambo la faraja kwamba katika mikutano mikubwa iliyotangulia, ikiandaliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa mikoa ya Mara na Dar es Salaam, mambo yalikwenda vizuri.

Hakika watu baada ya katazo hilo kuondolewa, walitarajia mtikisiko mkubwa kwenye mikutano hiyo na hata wengine wakitabiri ghasia, kutokana na hamu na shauku ya muda mrefu, wakiamini watu wangefurika na kukosa udhibiti.

Lakini, Jeshi la Polisi lilitenda wajibu na haki kwa kusimamia vema mikutano hiyo, ikiwa ni pamoja na kusindikiza viongozi wakuu wa CHADEMA kwenye makazi yao.

Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe akiwa Kanda ya Ziwa, alisindikizwa kwa ving'ora kama ifanyavyo kwa viongozi wa kitaifa, hali kadhalika Makamu wake, Tundu Lissu akiwa Dar es Salaam.

Hiyo ni ishara kuwa mikutano hii iliyotokana na mazungumzo ya maridhiano yaliyoendeshwa na Rais Samia na vyama vya siasa, imeweka mazingira rafiki ya kisiasa nchini na kila mpenda amani anatarajia hali hiyo kushamiri.

Changamoto kubwa inayojidhihirisha zaidi Dar es Salaam, tofauti na mikoani, ni maeneo ya kufanyia mikutano hiyo, ambayo itaendelea kuvuta umati mkubwa wa watu na hivyo kuhitaji ulinzi imara.

Sasa utakuwa mzigo mkubwa kwa Jeshi la Polisi, chini ya Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, kwani dhima yake ni kuhakikisha kila aendaye mkutanoni, anafanya hivyo na kurejea nyumbani salama.

Kwa kuwa naye ameanza kwa mguu mzuri na kutoa taswira njema kwa wadau wa siasa nchini, bila shaka hata kuwa tayari kuona wananchi wanaumia chini ya ulinzi wake, hivyo anahitaji ushirikiano wa wadau wengine.

Miaka yote ilizoeleka, viwanja vya Jangwani na Mnazi moja, Ilala, Dar es Salaam kuwa mahali maalumu pa kufanyia mikutano hiyo na hata wakati mwingine matamasha ya michezo na fani zingine za kimaisha. Leo hii, Jangwani hapatazamiki kabisa, pamegeuka vichaka na mashamba, mahali ambako kampeni za Uchaguzi Mkuu Mwaka 2020 zilifanyika bila matatizo kwa vyama vyote vya siasa vilivyopenda kufanyia hapo, pamefunikwa majani na miti.

Mnazi Mmoja, mbali ya kuwa sehemu ndogo isiyoweza kuhimili umati wa watu wa mikutano ya kisiasa, pamezungukwa na biashara, hivyo likitokea la kutokea, biashara za watu mbalimbali zinaweza kuathirika na kusababisha tafrani isiyohitajika.

Mahali kwingine ambako wanasiasa walipatumia sana kwa mambo hayo ya kisiasa, ni viwanja vya Mwembe Yanga, Temeke. Nako leo kuna ujenzi unaendelea na ndiyo sababu hata CHADEMA wakaamua kufanyia eneo la Bulyaga, Temeke Wailes, ambako ni finyu na katikati ya makazi ya watu.

Eneo la Kawe maarufu kama Tanganyika Packers, ni viwanja ambavyo pia vilitumika kwa kampeni na mikutano mingine ya kisiasa, lakini leo pamegubikwa na mikutano ya ibada.

Mbagala Zakhem nako kulitumiwa na wanasiasa kwa mikusanyiko ya aina hiyo, hivi sasa kumejengwa soko na kituo cha mabasi, hivyo kupoteza sifa ya kuwa eneo la kufanyia mikutano.

Sehemu nyingine iliyokuwa kwa ajili ya mikutano; Kwa Bakhressa, Manzese, Kinondoni, ambako kwa sasa kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea hapo, eneo limepungua.

Viwanja vya Kigogo Sambusa, Ilala, nako hivi sasa kuna soko na yadi ya kokoto kwa ajili ya ujenzi, huku viwanja vya Biafra nako kukigeuka maegesho ya mabasi ya kukodi, ilhali pia ujenzi ukiendelea na mnada kufanyika hapo mara mbili kwa wiki.

Pengine kwenye klabu ya viongozi; Leaders Club Kinondoni, ambako nako palivyo sasa kwa mikutano ya hadhara kama ya CHADEMA na CCM kufanyika, kwa kuzingatia wingi wa wafuasi wanaona kunahitajika maeneo mengine.

Kwa sasa, si rahisi serikali ikatenga fedha kwa ajili ya kuandaa viwanja vya wazi kwa wanasiasa, licha ya kuruhusu mikutano hiyo, hususan kwa Jiji la Dar es Salaam. Pengine sasa itolewe ruhusa ya kutumia viwanja vya michezo vya Benjamin Mkapa, Uhuru, Karume na Azam Complex kwa ajili hiyo, lakini kwa malipo fulani ya kusaidia kuvitunza. Vinginevyo, mikutano hii itafanywa kwa kujibana au kwa idadi fulani ya washiriki.

Hili linaweza kuwa jambo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini. Hata hivyo, tuendelee kufanya mikutano, lakini kwa amani, utulivu, staha na upendo. Alamsiki!

UCHUMI

# Darasa la UTT AMIS kwa wote 'pa kutokea' kupitia uwekezaji



Shughuli za kibiashara zikiendelea. Suala la faida linashauriwa kuwapo busara stahiki katika matumizi na uwekezaji endelevu. **PICHA: MTANDAO.**

**NA MWANDISHI WETU**

MIKAKATI ya kufikia maendeleo kiuchumi ina sura nyingi, ikiwamo kuwekeza, kuzalisha na kutanua wigo wa masoko binafsi.

Kitaalamu inaelezwa mbinu za kuwekeza hasa fedha ziko nyingi, ingawa wapo wengi wanashindwa kuzitambua ili kufikia mafanikio kwa maisha ya muda mrefu.

Inaelezwa kwamba, mara zote kabla ya mtu au taasisi kufanya uwekezaji, anapaswa ajiulize maswali kadhaa yakiwamo, namna anavyotumia kipato chake na kiulizo binafsi; Je, pato langu linatokana na nini?

Fikra binafsi kuhusu fedha apatazo mtu inatajwa ni muhimu. Wapo ambao wakipata fedha, wanajikita kwenye starehe, kila mmoja na utashi wake, iwe pombe, mavazi na mengineyo.

Marejeo ya kibusara ni kwamba, fikra hizo zipo sahihi? Ili kufanikisha hayo, kuna hoja ya kisaikolojia haja ya kuwa na kapu la fedha lenye mchanganyiko utakaosaidia maisha ya kila siku, pia baadaye.

Mahitaji ni mengi! Kapu linapaswa kuwa na fungu la dharura walau hela ya mahitaji muhimu ya miezi mitatu hadi sita, iwapo mhusika hatakuwa na kipato, ingawa upande wa pili wa shilingi kutoka uhalisia, unatajwa ni ngumu kutekeleza.

Cha lazima katika hilo, ni walau kipato cha lazima kinachogusa chakula, mavazi, malazi, tiba na elimu kiwe nusu ya akipatacho mtu; mahitaji yasiyo ya lazima kundi la starehe na burudani yapewe asilimia 30; na akiba na uwekezaji ushike asilimia 20.

**INAKOSIMAMA UTT**

Hapo ndipo kunaangukia aina ya uwekezaji unaoshauriwa kwenye hisa kama, vipande vya taasisi ya kifedha ya UTT AMIS, hati fungani za serikali, kampuni binafsi na maeneo ambayo baadaye fedha hiyo inakuwa mtaji maalum.

UTT imeunda vikapu vilivyopo; kimoja cha matumizi ya mwezi na kingine fedha ya matumizi ya milele kidumu, hata baada ya uhai wa mwekezaji.

Hapo panatajwa hata baada ya mwekezaji kuaga dunia, kunakuwapo maisha yanayoendelea kwa maana ya miradi ya kifamilia inayodumu.

Kapu jingine ni fungu la dharura, ambalo halina maisha marefu. Mara nyingi kinakuwa ni matumizi ya muda mfupi; mwezi mmoja hadi sita kulingana na hali ya familia.

Pia, UTT ina kapu la maisha ya milele; huo ni mpango wa milele, kwa sababu kunawezekana kuwa hata baada ya ukomo wa uwapo hapa duniani kinatakiwa kiwepo.

Ni kapu linalohusisha watu wa karibu – warithi, familia na watoto huwa warithi na sehemu ya mpango, kwa namna mbalimbali.

UTT AMIS inashauri njia sahihi ya kuzifikia ni kuwekeza kwa kununua hati zake fungani au vipande na ili kufanikiwa, mtu anapaswa ajiwekee bajeti ya matumizi akijielekeza kwenye malengo binafsi.

Kanuni inayoshauriwa na UTT ni mgawanyo wa kipato uliotajwa awali (kwa asilimia); 50-30-20. Maana yake nini? Ishara yake ni katika tija ya mfano, mtu anapopata kipato shilingi milioni moja, ina maana inaangukia mgawanyo, Sh. 500,000 inaangukia mahitaji muhimu; Sh. 300,000 kwa mahitaji yasiyo ya lazima; kisha Sh. 200,000 akiba ya uwekezaji.

Uwezo wa kifamilia nao unatofautiana, zipo zenye kipato kikubwa, wanawekeza zaidi na wa kipato kidogo, wanabaki chini.

Kapu la mipango ya baadae, pia huendana na hali ya soko la fedha, kwa mfano mtu anaweza kuwekeza na kisha fedha zikapotea, kulingana na kasi ya mfumuko wa bei ulikosimamia.

**KINACHOSHAURIWA**

Daima inashauriwa, mtu ajenge mazoea ya kutembelea na kukagua nyendo na mipango ya kisoko kwenye benki tofauti, kwani zinatofautiana.

Kwa kawaida, faida ya uwekezaji kwa wamiliki wa vipande vya UTT AMIS, hupatikana kwa mfumo wa gawio la mapato na kukua mtaji unaotokana na uwekezaji wa pamoja.

Kuna faida kubwa mtu anaweza kuipata kwa kuwekeza katika mifuko inayosimamiwa na taasisi hiyo, kama vile uwekezaji wa kutawanya, unaopunguza hatari ya uwekezaji na kuongeza mapato.

# Mbunge wa kike mwenye rekodi ya makubwa kuwapigania kinamama

**INATOKA UK.11**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliunda tume ya kuchunguza suala hilo na baadaye, bei ya chai ilipanda kutoka Sh, 132 hadi Sh, 300 kwa kilo.

Hata hivyo, Sophia analalamika kuwa, bado bei hiyo ni ndogo, ikilinganishwa na chai inayovunwa kwenye wilaya za Njombe na Lushoto mkoani Tanga.

Mazao mengine aliyoyavalia njuga anayataja ni pamoja na kokoa ambayo imepanda bei kutoka shilingi 2000 za awali na kufika Shilingi 5000, huku parachichi ikiuzwa shilingi 1800 kutoka Shilingi 1,000 za awali kwa kilo. Anasema, kutokana na mkoa wa Mbeya kuwa na mvua za kila mara, mbunge huyo anajinasibu kwamba, amewawezesha wanawake wajasiriamali kupatiwa miamvuli mikubwa ya kujikinga na mvua wakati wote.

Pia, anasema ametumia nguvu kubwa kuweka msukumo wa kuhakikisha pato la kisheria la asilimia 10 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe linawafikia walengwa ambao ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Sambamba na hilo, Sophia anajigamba kuwa wanawake hao wajasiriamali wameweza kupata mikopo kupitia benki na kampuni.

**CHANGAMOTO KIUCHUMI**

Sophia anawaomba walioko kwenye sekta binafsi, nje na ndani ya mkoa wa Mbeya, kuwekeza kwenye miradi ya kiuchumi inayotembea kwenye mnyororo wa wakulima.

Anatoa mfano wa wafugaji ng'ombe wanaolia na bei ndogo ya maziwa ya Shilingi 600 kwa lita, kwamba haiwasaidii kupunguza makali ya maisha, akipendekeza walau ifike bei ya shilingi 1000 kwa lita, endapo wawekezaji wengi wangejitokeza kuwekeza kuliko ilivyo sasa.

Hata hivyo, mbunge huyo anaipongeza serikali kwa upande wa hospitali, vituo vya afya na zahanati zinazojengwa kwa kasi katika maeneo mbalimbali mkoani Mbeya.

Anaitaja Hospitali ya Makandana, Kituo cha Afya Ikuti, Masikulu na Kiwira, huku akiikumbusha serikali kupeleka vifaa na watumishi katika baadhi ya zahanati zenye upungufu huo.

Kuhusu miundombinu ya barabara, Sophia anasema kwa kushirikiana na wabunge wenzake mkoani Mbeya, wamesaidia upatikanaji wa fedha za ujenzi wa barabara mbalimbali.

Anazitaja baadhi yake ni barabara za Igawa wilayani Mbarali hadi Tunduma mkoani Songwe; Uyole hadi Kyela (Mbeya); na Busokelo hadi Katumba wilayani Rungwe, zilizoko kwenye utekelezaji.

Kwa sasa, anaomba serikali kuiongezea fedha Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), imudu kupunguza changamoto za barabara zilizopo maeneo ya pembezoni, ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao kwa haraka na uhakika zaidi.



## Jingu ahimiza ushirikiano watumishi Ofisi ya Waziri Mkuu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera Bunge na Uratibu, Dk. John Jingu, amewataka watumishi wa ofisi hiyo kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuwa na utendaji wenye matokeo chanya.

Dk. Jingu aliyasema hayo juzi jijini hapo, alipokuwa akizungumza na watumishi kwenye mkutano kwa ajili ya kuwajengea uelewa kuhusu mada masuala ya afya ya akili, magonjwa sugu yasiyoambukizwa na ulaji usiofaa pamoja na maadili mahali pa kazi.

Katibu Mkuu huyo aliwasisitiza watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi na kushirikiana kwenye maeneo yao ya kazi,ili kuyafikia malengo ya serikali kwa ujumla na kujiletea maendeleo.

Alisema kuwa ipo haja ya kuwa na mafunzo kwa kila mtumishi kwa kada zote ili kuwajengea uwezo utakaoleta tija katika kutekeleza majukumu yao.

Alifafanua kuwa vikao vya idara na vitengo kila wiki vitasaidia kupata uelewa wa pamoja juu ya majukumu waliyonayo ambayo yatasaidia kuongeza ushirikiano na uwezo katika utendaji kazi wa kila siku.

Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Waziri Mkuu, Numpe Mwambenja aliishukuru ofisi kwa kuandaa mkutano huo, huku akisisitiza watumishi kuendelea kutekeleza majukumu kwa ushirikiano ili kuweza kutimiza malengo.

# Jafo: Sijaridhishwa na kasi ujenzi jengo la Makamu wa Rais

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo amekagua ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais unaoendelea katika eneo la mji wa kiserikali Mtumba akionyesha kutoridhishwa na maendeleo ya ujenzi huo.

Jafo alifanya ukaguzi huo akiwa ameongozana na viongozi na wataalamu kutoka ofisi hiyo.

Kwa mujibu wa mpango kazi uliowekwa, ujenzi huo kwa ujumla uko nyuma kwa siku 41 hali inayotokana na kasi ya ujenzi wa jengo hilo kuwa ya kutoridhisha.

Kutokana na hali hiyo Jafo alitoa wiki mbili kwa mkandarasi Kampuni ya SUMA JKT pamoja na Msimamizi Elekezi Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuhakikisha wanakamilisha kazi ya kusiliba (plasta) kuta ambayo ilipaswa kuwa imekamilika.

Alisema pamoja na kuwa wameaminiwa na kupewa dhamana ya ujenzi wa jengo hilo la serikali lakini hawajaonesha umakini katika utekelezaji wa mradi huo.

"Hapa mko nyuma sana wenzenu kule wako mbali sana kuliko ninyi na mara ya mwisho tulipokutana mkaniambia kazi itaenda kwa kasi lakini ndio mkaamua kabisa kusimama na mmeanza tena kufanya baada ya kusikia ninakuja kukagua, hapa naona hakuna umakini katika kufanya hii kazi," alisema Jafo.

Aidha, alisema serikali haitavumilia kuona kazi hiyo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais inakwama na kuwa kama hawataonesha maendeleo mkataba utavunjwa ili apewe mkandarasi mwingine atakayefanya kazi hiyo.

Katika ziara hiyo Waziri Jafo pia alitembelea majengo mengine yanayojengwa na SUMA JKT na kubaini ujenzi wake unakwenda kwa kasi hivyo akaonya kuchukua hatua ya kuvunja mkataba.

Ofisi ya Makamu wa Rais ilisaini mkataba wa Sh. bilioni 18.8 na Kampuni ya ujenzi ya SUMA JKT Oktoba 13, 2021 na kutakiwa kukamilisha kazi hiyo Novemba 09, 2023.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo (kushoto), akizungumza wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, eneo la mji wa kiserikali Mtumba, jijini Dodoma juzi. **PICHA: OMR**

# Masauni afanya ziara ya kushtukiza Kituo cha Polisi Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, amefanya ziara ya kushtukiza katika Kituo cha Polisi Dodoma kwa ajili ya kufuatilia utendaji kazi kituoni hapo.

Masauni aliwasili kituoni hapo juzi majira ya saa 6:02 mchana na kuwakuta wananchi eneo la mapokezi ya kituo hicho ambao walifika kwa ajili ya kuwachukulia dhamana ndugu zao waliopo katika mahabusu ya kituo hicho.

Akiwa kituoni hapo aliwahoji wananchi hao kama wanapata huduma nzuri kutoka kwa askari wa kituo hicho.

Pia akiwa katika mapokezi ya kituo hicho, alikagua kitabu cha taarifa za watuhumiwa wote waliopo mahabusu na baadaye kuelekea katika mahabusu hiyo na kuwaita baadhi ya mahabusu na kuwahoji kwa kuwaita kwa majina kujua makosa yao yaliyowafanya wawepo kituoni hapo.

Kabla ya kuzungumza na mahabusu hao, Masauni aliwataka wananchi wote waliofika kituoni hapo wakusanyike na kusikiliza kama wanamalalamiko yoyote ya kutohudumiwa vizuri au kero yoyote wanayotaka waziri aifahamu.

Mkuu wa Kituo cha Polisi hicho, OCS Namala Samson aliongoza kuwakusanya wananchi hao ambapo waziri aliwataka waseme kama kuna kero yoyote ya kupata huduma kituoni hapo.

Mkazi wa Nzuguni, Isaya Mwaiga alisema Polisi Dodoma wanafanya kazi nzuri licha ya kero wanazokabiliana nazo, ikiwemo karatasi moja wanaandikia watuhumiwa zaidi ya wawili na kuomba wasaidiwe ili wafanye kazi vizuri.

"Polisi Dodoma wanafanya kazi nzuri sana, Jana nimekuja kumtolea dhamana rafiki yangu, kwa muda niliokaa hapa nimejifunza kitu, kwanza vitendea kazi vya polisi, hususani karatasi moja wanaandikia watu wawili watatu, wanahangaika sana.

'Kama waziri mwenye dhamana tunakuomba uwatazame Jeshi la Polisi kuanzia hapa Dodoma mpaka nchi nzima, tupo katika kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi, lakini hawa pia wanasimamia ilani ya mama iweze kusimamiwa vema, wakitengenezewa mazingira mazuri ya kutoa huduma nzuri hata sisi mambo yetu yataenda vizuri" alisema Mwaiga.

Mkazi wa Kizota, jijini Dodoma, William Rashid alisema alifika kituoni hapo kumchukulia dhamana mke wake ambaye alifikishwa hapo kutokana na masuala ya vikoba lakini huduma ya dhamana ameipata bila kikwazo chochote.

Kadhalika, aliiomba serikali kukiboresha kituo hicho ambacho hivi sasa ni kidogo ukilinganisha na idadi ya wananchi wanaohitaji huduma kwa sasa jijini hapa.

Mkazi wa Michese, jijini Dodoma, Sostenes Mazengo amesema alifika kituoni hapo kumuombea dhamana ndugu yake lakini mlalamikaji hajafika, hivyo amemuomba Waziri huyo kusaidia endapo mlalamikaji anashindwa kufika watu waweze kusaidiwa kuliko kukaa muda mrefu kituoni.

Akizungumza na wananchi hao baada ya kuwasikiliza, Waziri Masauni alisema alikuwa anapita katika eneo hilo akaamua kupita kituoni hapo kusikiliza wananchi na kukagua utendaji kazi wa Polisi.

"Nilikua napita hapa, nikaamua kuja kusikiliza wananchi na pia kukagua utendaji kazi, mmetoa maoni yenu mimi nimefarijika sana, hata wananchi mliopo hapa mnaridhika chombo ninachokisimamia mnaridhika na jinsi wanavyotekeleza majukumu yao, nataka niwahakikishie kutokana na changamoto za askari, Rais Samia tangu aingie madarakani amefanya mambo mengi sana kuboresha Jeshi la Polisi," alisema Masauni.

"Hata jana ameunda tume kama mnafuatilia vyombo vya habari, pamoja na mambo mengine itaangalia maslahi ya askari matumizi ya mifumo ya kisasa, wakati mwingine unaweza ukalaumu askari kwa sababu hawana nyenzo, anaweza akapita mhalifu lakini wakiwa na mifumo mizuri ya kuhudumia kwa haraka pengine wangeweza kufanikisha majukumu yao, kwa kipindi cha muda mfupi mtaona mabadiliko makubwa katika Jeshi letu la Polisi." Masauni aliongeza kuwa Rais Samia ameongeza ajira katika majeshi, ameboresha vitendea kazi na pia Jeshi la Polisi lipo katika hatua ya mwisho ya ununuzi wa magari kwa wilaya zote nchini na ametoa Sh. bilioni 15 kwa ajili ya kununua magari hayo.

Pia alisema ujenzi wa vituo vya polisi umeanza na pia ujenzi nyumba za makazi unaendelea pamoja na kujenga vituo vya polisi nchini, pia amewapandisha vyeo askari na tangu aingie madarakani amewavisha vyeo askari wengi ambao ni zaidi ya 34,000 na mwaka huu watapandishwa wengine.

Hata hivyo aliwapongeza askari hao kwa kufanya kazi nzuri na amewapa moyo kwa waliyosema wananchi hao, na kuwataka waendelee kufanya kazi nzuri zaidi na kwa uzalendo na Rais Samia yupo pamoja nao katika kuwaboreshea mazingira ya kazi.



# Serikali yaanza 'vita' dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya, imeanza kutoa mafunzo maalum ya namna ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza kwa madaktari, wauguzi na wakunga ili kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya magonjwa hayo.

Mafunzo hayo yanafanyika kwa awamu katika kanda mbalimbali nchini ambapo wadau wanaoshiriki ni pamoja na Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Chama cha Madaktari wa Kisukari nchini.

Kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, mafunzo hayo yalifanyika kwa siku tatu na kuhitimishwa juzi jijini Mbeya ambapo watumishi wa afya kutoka katika mikoa mitano ya Mbeya, Iringa, Njombe, Rukwa na Katavi walishiriki.

Mwakilishi wa Chama cha Kisukari nchini, Dk. Rachael Nungu alisema waliamua kuanza kutoa mafunzo hayo ili kupunguza kasi ya magonjwa hayo nchini.

Alisema magonjwa hayo yamekuwa yakiigharimu serikari fedha nyingi wakati wa kuwatibu wananchi wanaougua huku akisisitiza kuwa ili kuyaepuka ni lazima wananchi wabadili mfumo wa maisha.

Alisema magonjwa hayo yanatokana na mifumo ya ulaji usiozingatia lishe bora, kutokufanya mazoezi, unywaji wa pombe kupita kiasi na uvutaji wa mazao ya tumbaku ikiwemo sigara na shisha.

"Utafiti uliofanyika hivi karibuni ulionyesha kwamba asilimia 21 ya bajeti inayotengwa na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ambayo inatengwa kwa ajili ya kutibu magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza hutumika kutibu magonjwa mawili pekee ambayo ni Shinikizo la juu la damu na kisukari," alisema Dk. Rachael.

Mwakilishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Ansbert Kakigira aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kwenda kutekeleza mipango ya kukabiliana na magonjwa hayo kwenye vituo vyao kwa kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na magonjwa hayo.

Aliwataka wataalamu hao kuisaidia serikali kuboresha huduma kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi hasa kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma zinazostahili zikiwemo za matibabu ya magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza.

Aliwataka waliopata mafunzo hayo kwenda kutoa elimu waliyoipata kwa wenzao ambao hawakupata nafasi kwa maelezo kuwa baadaye kutakuwepo na usimamizi shirikishi. "Tunachotaka sasa hivi ni kwamba haitakiwi mtu mwenye uzito uliopitiliza apelekwe Hospitali ya Taifa Mhimbili kwenda kuwekewa puto, tunataka aanze kupata huduma huku chini kwahiyo haya mafunzo ni muhimu sana kwenu," alisema Dk. Kakigira.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema awali walikuwa hawana uelewa wa kutoka kukabiliana na magonjwa hayo lakini baada ya kufundishwa wanakwenda kuwasaidia wananchi.

Mmoja wa washiriki hao, Hamida Ngakonda kutoka mkoani Iringa alisema mafunzo hayo yamewasaidia kupata nyenzo muhimu ya kwenda kubadili mfumo wa maisha kwa wananchi.

Akifunga mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji alipongeza serikali kwa kuanzisha mafunzo hayo kwa maelezo kuwa magonjwa hayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi nchini.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kwenda kuleta mabadiliko kwenye jamii kwa maelezo kuwa kuna uwezekano wakaleta mabadiliko kwa kutumia mafunzo hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, Josephine Manase (kulia), akikagua kitalu cha miche ya michikichi, wilayani humo juzi, iliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) kwa ajili ya kuendeleza zao hilo kabla ya kugawa baadhi ya miche kwa wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# H'shauri yafanya usafi sokoni, makazi

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imeanzisha utaratibu wa kufanya usafi usiku na mchana ili kukabiliana na tatizo la uchafu uliokithiri kwenye maeneo mbalimbali yakiwemo ya kwenye masoko na kwenye makazi ya watu.

Meya wa Jiji hilo, Sheikh DorMohamed Issa aliyasema hayo juzi alipozungumza na wandishi wa habari kuhusu mikakati ya kulifanya Jiji hilo kuwa safi pamoja na kuepuka magonjwa ya mlipuko kikiwemo kipindupindu.

Alisema awali usafi ulikuwa unafanywa moja kwa moja na halmashauri kwa kutumia maghuba yaliyokuwa yamesambazwa kwenye maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa yanasafirishwa kwenda ghuba kuu kwa kutumia magari maalumu.

Alisema kwa sasa shughuli hiyo imerejeshwa kwa wananchi kupitia viongozi wa kata ambako wameelekezwa kutafuta wazabuni wa kutekeleza kazi hiyo ya usafi.

Alisema usafi ukifanyika mchana magari ya kuzoa taka yanachelewa kufika kwenye dampo kuu kutokana na msongamano wa magari barabarani.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga alisema kwa sasa mapato yote ya taka yanakusanywa kwenye kata na kupangiliwa na viongozi wa maeneo hayo.

Alisema awali usafi ulikuwa unafanywa na Jiji ulikuwa unachochea maeneo mengi kuwa machafu kutokana na wananchi kutokuwa na utaratibu mzuri wa kumwaga taka hizo ambapo walikuwa wanamwaga hata chini.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliwataka viongozi wa halmashauri hiyo kuongeza juhudi za ufanyaji wa usafi wa mazingira pamoja na kulinda vyanzo vya maji.

# Mkakati kuwanusuru wananchi vumbi la makaa mawe waanikwa

**Na Augusta Njoji**

OFISI ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imetaja mikakati mbalimbali iliyochukuliwa kwa lengo la kuwanusuru wananchi wa Mtwara dhidi ya vumbi la makaa ya mawe.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Hamza Khamis Chilo aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Anastazia Wambura.

Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kuwanusuru wananchi wa Manispaa ya Mtwara dhidi ya vumbi la makaa ya mawe.

Naibu Waziri Chilo alisema serikali tayari imeshachukua jitihada za kuweka miundombinu ya kupunguza vumbi la makaa ya mawe ili kuwanusuru wananchi.

"Tayari Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imefunga mfumo wa dust suppression system (mfumo wa uondoaji wa vumbi) unaotumia maji kupunguza vumbi.

"Pia limetengwa eneo maalum kwa ajili ya kujenga 'Conveyor belt' itakayotumika kupakia makaa ya mawe kwenye meli," alisema.

Naibu Waziri huyo pia alisema limetengwa eneo maalum nje ya mji takribani kilomita 34 kwenye Kijiji cha Kisiwamgao kutoka mjini Mtwara kwa ajili ya kuhifadhi mizigo ya namna hiyo na kusaidia kupunguza kusambaa vumbi kwenye mazingira.

"Ninapenda kumhakikishia mheshimiwa mbunge kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia NEMC (Baraza la Taifa la Udhibiti na Uhifadhi wa Mazingira) kwa kushirikiana na Manispaa ya Mtwara na TPA kwa pamoja tunaendelea kufuatilia na kusimamia wasafirishaji wa makaa ya mawe ili wazingatie taratibu za kuhifadhi mazingira kwenye maeneo yote," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema bandarini kwa sasa kuna maji yametuama meusi yanayotokana na vumbi hilo na kuhoji mkakati wa serikali wa kuhakikisha inatunza na kulinda vyanzo vya maji ili visiathiriwe na maji ya mvua yanayotiririka yenye vumbi hilo.

"Serikali itakuwa tayari kupokea ushauri kwamba haya makaa ya mawe yakitoka kwenye migodi yafungwe kwenye vifungashio?" mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Chilo alisema sheria inaelekeza watu na kampuni zinazofanya shughuli zinazogusa vyanzo vya maji, kuvitunza.

Alitoa wito kwa Watanzania kutunza vyanzo vya maji na kwa watakaokiuka, sheria na taratibu zitachukuliwa dhidi yao.





# Dk. Mwinyi aiomba Russia kusaidia sekta ya afya, utalii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiomba Serikali ya Russia kuisaidia Zanzibar kwenye sekta za afya, utalii na uchumi wa buluu.

Alitoa ombili hilo jana Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na Balozi wa Urusi nchini Tanzania, Andrey Avestisyan.

Dk. Mwinyi alisema uhusiano wa kidiplomasia baina ya Russia na Zanzibar ni wa undungu na historia na kueleza kwamba Watanzania wengi wakiwamo Wazanzibari wako nchini Urusi kwa ajili ya masomo .

Alisema serikali anayoiongoza imeimarisha sekta ya afya kwa kujenga hospitali kubwa za wilaya na mikoa, hivyo aliomba ushirikiano wa kupatiwa madakrati bingwa kwenye hospitali hizo na fursa ya madaktari wa Zanzibar kwenda Russia kwa ajili ya kuongeza ujuzi na utaalamu.

Akizungumzia sekta ya utalii, alisema Zanzibar ina fursa nyingi na vivutio adhimu, hivyo alimuomba balozi huyo kuangalia uwezekano kwa kuleta watalii wengi zaidi ili pande zote mbili zinufaike na fursa hizo.

Alisema Zanzibar imejaaliwa baraka ya visiwa vizuri vyenye mvuto kwa utalii na ardhi ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji wa sekta hiyo, pamoja na Mji Mkongwe ambao ni kivutio adhimu kwa wageni wanaofika visiwani.

Hivyo alimkaribisha Balozi Avestisyan kuitumia fursa hiyo kuwakaribisha wananchi wa Urusi kufika visiwani Zanzibar kujionea tunu.

Naye Balozi Andrey Avestisyan, alisema ushirikiano baina ya nchini mbili hizo mbali na kuimarisha umoja wao lakini kuangalia fursa ya kuwaleta Warusi wengi Tanzania hasa visiwani Zanzibar kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya utalii na uchumi wa buluu.

Alisema endapo watafanikiwa kuwashawishi wawekezaji wa Russia kuja kuishi na kuwekeza Zanzibar kutakua na haja ya kuanzisha ubalozi mdogo wa Russia, Zanzibar suala alilolieleza kwamba washaanza mazungumzo nalo na serikali ya nchini kwake.

Alisema katika kudumisha ushirikiano uliopo baina ya Russia na Zanzibar, itawapendeza zaidi kuanzisha safari za ndege za moja kwa moja baina ya Russia na Zanzibar hali aliyoieleza itasaidia Warusi wengi kutalii Zanzibar na kuvutiwa na mandhari mwanana ya upepo wa visiwa.

Kuhusu uchumi wa Buluu, Balozi Andrey, alisema Warussia wengi wana utaalamu mkubwa wa kusarifu masuala ya uvuvi na matunda ya bahari na kueleza kwamba eneo hilo watalichukulia kwa umuhimu wa pekee katika kuimarisha sekta hiyo.

Kuhusu sekta ya afya, alisema wataleta madaktari kuja kutoa mchango wao kwa Zanzibar lakini pia watatoa hamasa kwa wageni wa kitalii na wawekezaji kutoka Russia kuona kwamba watatibiwa na madaktari bingwa kutoka nchini mwao.

Uhusiano wa diplomasia baina ya Tanzania na Russia ulianza Desemba 11 mwaka 1961 ambapo Tanzania ilianzisha ubalozi wake kwenye Mji Mkuu wa Russia, Moscow na Russia ilianzisha ubalozi wake jijini, Dar es Salaam.

Zaidi ya Watanzania 3,000 wako Russia wakiendelea na masomo yao kupitia fani mbalimbali.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikabidhi zawadi ya mlango wa Zanzibar kwa Balozi wa Russia nchini, Andrey Avetisyan, baada ya mazungumzo yao, Ikulu jijini Zanzibar juzi, alipofika kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: IKULU**

## Kamati yabaini ukiukwaji sheria ya manunuzi ya bidhaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAC) imesema imebaini ukiukwaji wa sheria za manunuzi ya bidhaa mbalimbali za serikali hali iliyoisababishia hasara serikali.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Habib Ali Mohamed wakati akizungumza na watendaji wa wakala wa manunuzi na maofisa wa manunuzi wa Serikali ya Zanzibar.

Alisema serikali imeanzisha sheria ya manunuzi kwa ajili ya kuwepo kwa utaratibu utakaofuatwa kwa mujibu wa sheria ya kufanya manunuzi yote ya mali za serikali ikiwamo kuwepo kwa risiti.

Alisema utafiti umebaini kwamba watendaji wengi hawafuati utaratibu huo wakifanya hivyo kwa makusudi kwa ajili ya kuikosesha serikali mapato yake yanayotokana na manunuzi ya mali za umma.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Ali Suleiman Ameir, alisema serikali ipo katika mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi baada ya kubaini mapungufu mengi ambayo ni kikwazo katika kuyafikiya malengo yaliyokusudiwa.

Alisema kwa mujibu wa taarifa za wakaguzi wa ndani wa mahesabu wamebaini kuwepo kwa kasoro nyingi zinazotokana na watendaji wa serikali kushindwa kufuata sheria za manunuzi na hivyo kuikosesha serikali mapato yake.

Naibu Katimu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Aboud Hassan Mwinyi, alisema kuwepo kwa mifumo rasmi inayotumiwa na serikali katika ukusanyaji wa fedha utapunguza udanganyifu unaofanywa na wafanyakazi katika masuala ya manunuzi.

Alisema tayari Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA) imeanza kutumia mifumo rasmi ya ukusanyaji wa kodi katika vyanzo mbalimbali ikiwamo taasisi zinazofanya biashara za serikali.

# Tuzo za umahiri waandishi wa habari kutolewa mwezi huu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimeandaa tuzo za umahiri wa uandishi wa habari za takwimu na uongozi kwa wanawake mwisho wa mwezi huu.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi wa tuzo hizo, Dk. Mzuri Issa, alisema tayari jopo la majaji watakaochambua kazi za waandishi wa habari zilizowasilishwa limeanza kazi na linatarajia kumaliza Febuari 10, mwaka huu.

Alisema kazi hizo zitakazoshindaniwa ni za vyombo vya habari vya radio, magazeti, runinga na mitandao ya kijamii ambapo mshindi atapata zawadi mbalimbali ikiwemo fedha.

Alisema jopo la majaji watano limeanza kazi ya kuzipitia kazi za waandishii zilizowalishwa.

Aidha, alisema mashindano hayo yanafanyika kwa mara ya pili ambapo mara ya kwanza yalifanyika mwaka jana.

Alisema vigezo zilivyotolewa awali ni pamoja na makala hizo kuzingatia mada husika lakini pia kuwapo kwa ubunifu wa mada, habari iliyokuwa na vyanzo tofauti vya habari pamoja na makala au vipindi hivyo kuzingatia masuala ya jinsia na makundi ya pembezoni. "Mada kuu ya makala na habari ni lazima iwe imelenga katika suala la takwimu na uongozi wa wanawake lakini pia kuzingatia ubunifu, lugha fasaha na kufuata maadili ya uandishi wa habari,"alisema Dk. Mzuri.

Hata hivyo aliwataka majaji kuzingatia vigezo vya umahiri katika kuzifanyia uchambuzi makala zilizowasilishwa lakini pia kuzingatia usiri na uadilifu ili shughuli hiyo kufanikiwa.

Alisema nguvu ya vyombo vya habari haina budi kutumika katika kujenga jamii bora huku jinsia zote wanawake na wanaume wanapata fursa za kuwa viongozi katika nafasi za kitaaluma, kijamii, na kitaifa.

Tuzo hizo zinafanyika kupitia mradi wa kuwawezesha wanawake katika uongozi ambao unatekelezwa kwa pamoja na TAMWA Zanzibar, Jumuia ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) pamoja na Jumuia inayojihusisha na Mazingira,Usawa wa Kijinsia na utetezi Pemba (PEGAO) kwa kushirikiana na ubalozi wa Norway Nchini Tanzania.

Kauli mbiu katika sherehe hizo ni "kalamu yangu, mchango wangu kwa wanawake" ikiwa na lengo la kuhamasisha waandishi wa habari kutumia kalamu zao katika kuelimisha umma umuhimu wa nafasi za wanawake katika uongozi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHUKRANI MOHAMED BENARD** anatangaza kupotea kwa living certificate na cheti cha kidato cha nne chenye No. CS 172780 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia IBINZA SECONDARY SCHOOL Mwaka 2013. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.**TAARIFA YA POLISI: DOD/DOD/RB/482763/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAURENCE JACOB MGANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mitsubishi Fuso yenye namba za usajili T. 437 ASV. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Laurence Jacob Mganga kwa simu namba 0719651044. Taarifa ya Polisi

**MAS/RB/910/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NO. 3 YA MWAKA 2023**
**CANARA BANK TANZANIA LIMITED............MDAI**
**DHIDI**
**BRIBOS COMPANY LIMITED..............1. MDAIWA**
**VUHUNGU NGAJILO......................2. MDAIWA**
**SALOME DICKSON SAMEJI................3. MDAIWA**

**KWA:**
**BRIBOS COMPANY LIMITED**
**VUHUNGU NGAJILO**
**SALOME DICKSON SAMEJI**
**POPOTE WALIPO.**
**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya hati madai ambayo inapatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unaamriwa kuhudhuria katika Mahakama hii wewe binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 27/02/2023 saa 7:00 MCHANA mbele ya Mhe. F. MHINA PRM.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, inaweza kutoa hukumu dhidi yako kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 30 Mwezi JANUARI, 2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**
**SIMU YA UPEPO "UHAMIAJI"**
**OFISI YA AFISA UHAMIAJI MKOA,**

FAKSI +255 27 2642219
S.L. P 371,
SIMU +255 27 26 42219
TANGAA 30 JANUARY, 2023
KUMB: TA/IMM/70 VOL. II/6



**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**

**YAH: ANKITA DINSHKUMAR SUTAR**

Mwenye jina na picha hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh.Waziri wa mambo ya ndani ya nchi. Kwasasa ni raia wa india na ameolew na ndugu Dixit Hasmukh Sachania ambaye ni raia wa Tanzania na ni mfanyabiashara. Yupo hapa nchini tangu mwaka 2020 na katika kipindi chote hili ameishi mkoa wa tanga.

Kwa yeyotw mwenye taarifa/sababu za kwanini muombaji asipewe uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa kamishina jenerali wa uhamiaji S.L.P 1181 dodoma.

**Kny: KAMISHA JENERALI WA UHAMIAJI**

**IN THE JUVENILE COURT OF KOROGW**
**AT KOROGWE**
**CIVIL APPLICATION NO. 1 OF 2023**
**HAMADI OMARI DEGE............APPLICANT**
**MASEFU JERRY JAMES............RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on the 09 day of FEBRUARY, 2023 at 8:30 A.M. Before M.K. RASHID.

**YOU ARE** required to appear in this Court on the fixed date without fail.

**ALSO TAKE NOTICE** that in default of your Appearance on that the Case will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my hand and seal of the Court this 1 **Day of FEBRUARY, 2023**.

**IN THE DISTRICT COURT OF NZEGA**
**AT NZEGA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.1 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MICHAEL ANDREA MAGANGA ....... THE DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**
**JOHN AUGUSTINO PANGANI.............. THE PETITIONER**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 03 Day of MARCH, 2023

**Dated at Nzega this 31 day of January, 2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Shauri la madai /Ndoa Na. 69/2022**

Jina la mdai **MENGI LUSEGA LUBUWA**
Jina la mdaiwa **FESTO LITELEKO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama ya Mwanzo)

Kwa uje leo **FESTO LITELEKO** wa Mvomero

Kwa kuwa mdai/mdaiwa ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) uje kwa ajili ya kuanza ukumu kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 08/2/2023 saa.....asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyousu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa na Amri na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26 mwezi wa 01 mwaka 2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**

**TANGAZO KWA UMMA**

Halmashauri ya manispaa ya Morogoro inapenda kukutaarifu au mtu yoyote anayewafahamu **FRANK JOHN SAMBI** wa **S.L.P 67 MOROGORO** popote alipo kuwa ofisi imepokea maombi ya kumilikishwa kiwanja na **336 KITALU 'EE' AREA 6. KICHANGANI** kutoka kwa ndugu **ANASTAZIA THOMAS MBILANGO** ambaye ni msimamizi w a mirathi ya ndugu **FRANK JOHN SAMBI** wa **S.L.P 166 MOROGORO .**

Kwa taarifa hii ofisi inakupa siku ishirini na nane (28) ufike ofisini au kama kuna zuio lolote la kimahakama tufahamishe Ofisi ya Ardhi Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro . Vinginevyo ofisi itaendelea na taratibu za kuhamisha miliki ya kiwanja hiki na kumulikisha ndugu **ANASTAZIA THOMAS MBILANGO** ambaye ni msimamizi wa mirathi ya ndugu **FRANK JOHN SAMBI** wa **S.L.P 166 MOROGORO**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MWANAMVUA OMARI JUMA** anatangaza kupoteza kadi ya pikipiki yenye **No; MC 687 BVE** Yenye chassis No; **MD625AF73H1K04939**. **Eng. No; AF7KH1705224.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/6031/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DANISH MISSION TANGANYIKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili T 252 AJU. LENYE CHASSES NAMBA: JD0I5100509. Engine NoJDOJE2000530.Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/42998/2023.**

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Russia yajiandaa kwa shambulio kali

**KYIV, Ukraine**

WAZIRI wa Ulinzi wa Ukraine, amesema Russia inajitayarisha kufanya mashambulizi mapya makubwa na kuonya kuwa huenda yakaanza kesho.

Oleksii Reznikov, alisema Russia imekusanya maelfu ya wanajeshi na inaweza kufanya kitu kama kumbukumbu ya uvamizi wa awali mwaka jana.

Shambulio hilo pia lingeenda sambamba na Siku ya Watetezi wa Nchi ya Russia inayoadhimishwa Februari 3.

Wakati huohuo, watu watatu wamefariki katika shambulizi katika mji wa Kramatorsk.

Watu wengine wanane walijeruhiwa katika mji huo ulioko mkoa wa Donetsk baada ya kombora la Russia kushambulia jengo la makazi ya watu.

Gavana wa mji huo, alisema idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka huku waokoaji wakitafuta miili yao.

"Njia pekee ya kukomesha ugaidi wa Russia ni kuushinda," aliandika Zelensky kwenye mtandao wa kijamii kuhusu shambulio hilo.

Hivi majuzi Ukraine imetoa wito kupewa ndege za kivita kusaidia kujikinga na mashambulizi ya anga baada ya Ujerumani, Marekani na Uingereza kukubali kupeleka vifaru.

Reznikov alisema Russia ilikuwa imekusanya wanajeshi 500,000 kwa ajili ya mashambulizi hayo.

Mnamo Septemba, Rais Vladimir Putin alitangaza uhamasishaji wa jumla wa askari 300,000 walioandikishwa, ambao alisema ulikuwa muhimu ili kuhakikisha hadhi ya nchi.

Lakini,Reznikov alipendekeza kuwa takwimu halisi iliyosajiliwa na kupelekwa Ukraine inaweza kuwa kubwa zaidi.

"Rasmi walitangaza 300,000 lakini tunapoona wanajeshi kwenye mipaka, kulingana na tathmini zetu ni zaidi," aliuambia mtandao wa BFM wa Ufaransa.

Licha ya mapigano makali kuendelea katika eneo la mashariki la Donbas, vita hivyo vimeingia katika hali ya mkwamo katika miezi ya hivi karibuni tangu Ukraine kutwaa tena mji wa kusini wa Kherson.

Hatua ya kuchukuliwa kwa mji wa Soledar na Warussia hakuna upande ambao umepiga hatua kubwa kutwaa maeneo mengine.

*BBC*



Waokoaji wakiondoa vifusi kutafuta manusura katika jengo la ghorofa lililoharibiwa kwa kupigwa na roketi usiku wa kuamkia jana katika jiji la Kramatorsk, nchini Ukraine. **PICHA: AFP**

# Kanisa Orthodox lamuonya waziri mkuu

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

UONGOZI mkuu wa Kanisa la Kiorthodox nchini Ethiopia, unaojulikana kama Synodi, umetishia kuitisha mikutano ya kitaifa itakayoongozwa na mkuu wa Kanisa Hilo, Abuna Mathias.

Kanisa hilo limekosoa kauli za hivi karibuni za waziri mkuu kuhusu makasisi wakorofi waliohusika katika uteuzi wa maaskofu bila uelewa.

Katika hotuba yake ndefu, iliyotangazwa kwenye televisheni ya taifa, Abby alipinga sinodi ya kanisa hilo kuwatenga makasisi, ambao wanatoka katika jimbo la Oromia nchini humo.

Aliwaonya mawaziri wake dhidi ya kujihusisha na masuala ya kanisa.

Sinodi ilisema kuwa kauli za Waziri mkuu, zilipuuza maamuzi yake na kukosoa mamlaka yake na kulitambua kundi lisilo halali lenye njaa ya madaraka.

Kundi la maaskofu waliojitenga linalishutumu kanisa kwa kushikilia mfumo wa lugha na utamaduni na mamlaka tofauti.

Kanisa hilo upande wa Oromia waumini hawafundishi kwa lugha zao za asili.

Hata hivyo, kanisa hilo limekanusha shutuma hizo.

Makasisi waliojitenga walisema walizidiwa na uungaji mkono wa umma baada ya kutembelea baadhi ya maeneo katika jimbo lililokumbwa na mzozo la magharibi mwa Oromia.

Taarifa ya sinodi inakuja huku kukiwa na shutuma miongoni mwa waumini kwamba mamlaka zinawaunga mkono makasisi waliojitenga.

Uhusiano baina ya utawala wa Abiy na kanisa hilo lenye waumini karibu nusu ya milioni 110 ya raia wa Ethiopia, umekuwa ukizorota licha ya kwamba ulikuwa mzuri katika siku za mwanzo za uongozi wake.

Katika miaka ya hivi karibuni waumini wake wamekuwa wakiripotiwa kulengwa katika mgogoro huo.

Uhusiano wa pande mbili ulizorota zaidi wakati wa vita vya Tigray baada ya Askofu Abuna Mathias, kuzungumza dhidi ya kile alichokiita mauaji ya kimbari katika jimbo hilo.

*BBC*

## Papa Francis ateta na vijana DRC

**KINSHASA, DRC**

Kiongozi wa Kanisa Katoliki ulimwenguni Papa Francis, amekutana na maelfu ya vijana wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ikiwa ni sehemu ya ziara yake nchini humo.

Takriban vijana 80,000 walikutana na Papa, ambaye alilenga kuendelea kusambaza ujumbe wa amani na HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/papa-francis-awataka-wakongo-kusamehe/a-64580858" maridhiano baada ya juzi kukutana na wahanga wa madhila ya machafuko ya nchini humo.

Maelfu ya vijana walianza kuingia katika Uwanja wa Mashahidi ulioko mjini Kinshasa mapema asubuhi tayari kabisa kwa mkutano wa hadhara ulioongozwa na kiongozi huyo wa kiimani.

Uwanja huo ulifurika vijana kama 80,000 kwa ajili kusikia ujumbe utakaotolewa na Papa, aliyeko ziarani barani Afrika.

Karibu asilimia 60 ya watu nchini humo ni vijana wa chini ya miaka 20, ikiwa ni kulingana na takwimu za Umoja wa Mataifa.

Pamoja na mzozo unaoendelea kuwaathiri vijana, wengi pia hawana ajira.

Sheila Magumbu, mmoja ya vijana waliojitokeza uwanjani hapo alisema anatumaini kusikia ujumbe wa amani kutoka kwa Papa Francis, na hasa kwa ajili ya wakazi wa mji wa Goma ulioko mashariki mwa DRC.

Na kama ilivyo kwa Sheila, wengi wanaamini kwamba huo ndio utakuwa ujumbe mkuu ikiwa ni pamoja na maridhiano miongoni mwa watu wa taifa hilo ambalo mizozo imesababisha mamilioni ya watu kuuawa katika miongo kadhaa iliyopita, huku watu milioni 5.7 wakiwa hawana mahala pa kuishi baada ya kuyakimbia makazi yao.

*DW*

## Israel yashambulia Ukanda wa Gaza

**TEL AVIV, Israel**

JESHI la Israel limesema vikosi vyake vimeshambulia maeneo katika Ukanda wa Gaza, kujibu shambulio la roketi kutoka eneo hilo.

Katika taarifa yake kupitia mtandao wa Twitter, jeshi hilo la IDF limesema mashambulizi yake yalilenga kituo cha uzalishaji wa kemikali ghafi, pamoja na kituo cha utengenezaji silaha, ambacho kimesema kinamilikiwa na kundi la Hamas linalodhibiti ukanda huo.

Kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari ambazo hazijathibitishwa, ndege za kivita za Israel zilishambulia maeneo kwenye kambi ya wakimbizi katikati mwa Gaza. Masaa machache kabla ya shambulio la Israel, jeshi lilisema lilikuwa limezuwia roketi kutoka Ukanda wa Gaza.

HABARI MICHEZO

# SHIKANGWA AFUNGA HAT-TRICK AKIIPANDISHA SIMBA QUEENS

**Na Adam Fungamwango**

MABAO manne yaliyofungwa na mshambuliaji Mkenya aliyesajiliwa na Simba Queens katika dirisha dogo la usajili, Jentrix Shikangwa, yaliiwezesha timu ya yake kuwachapa wenyeji Alliance Girls mabao 4-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza juzi.

Ushindi huo ukaipaisha Simba Queens hadi katika nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake kwa kufikisha pointi 16 huku JKT Queens yenye pointi 17 ikiwa kileleni.

Hiyo ilikuwa ni 'hat-trick' ya pili kwenye ligi hiyo, ya kwanza ikiwekwa na mshambuliaji na nahodha wa Simba Queens, Oppa Clement.

Maafande wa JKT Queens wao walitoka suluhu na Yanga Princess, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam.

Tigers Queens ikichezwa kwenye uwanja wake wa Black Rhino ulioko Karatu, Arusha iliwatandika Amani Queens mabao 3-0 huku Mkwawa Queens iliyocheza mbele ya mashabiki wake ikichapwa mabao 3-0 na Baobab Queens.

Fountain Gate Princess ilitoka suluhu dhidi ya Ceasiaa Queens, mechi iliyofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Yanga Princess yenye pointi 14 iko katika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo wakati Alliance Girls ikichuka hadi nafasi ya tano ikiwa na pointi 10 ikifuatiwa na Baobab Queens, Ceasiaa, The Tigers Queens, Amani Queens na Mkwawa Queens ikiburuza mkia.




Kiungo wa Yanga Princess, Amina Ally (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa JKT Queens, Annastazia Katunzi katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

# Oscar, Mbega kumaliza ubishi

**Na Saada Akida**

BONDIA Oscar Richard atachuana na mpinzani wake wa muda mrefu, Adam Mbega katika pambano la utangulizi litakalofanyika Februari 24, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Pambano kuu siku hiyo litakuwa ni kati ya Selemani Kidunda dhidi ya Mkongomani, Patrick Mukala ambao watawania mkanda wa ubingwa wa Afrika (ABU).

Promota wa ngumi za kulipwa wa Kampuni Kemmo Sports Agency, Saadah Salum, alisema mabondia hao watawania mkanda wa ubingwa wa Taifa unaotambuliwa na Kmisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC).

Saada alisema lengo wa kuwapambanisha Oscar na Mbega kuwapa nafasi mabondia hao kumaliza 'ubishi' kutokana na tambo zao za muda mrefu.

"Tukiwa waandaji wa pambano la Kidunda na Mukala, tumeamua kuwajumisha kwa kuwapa nafasi Oscar na Mbega, hawa ni wapinzani wakubwa, wanatoka kwenye eneo moja, yaani hii ni dabi ya watu wa Mabibo, lakini pia ni pambano ambalo lilikuwa linasubiriwa kutookana na kutocheza kwa muda mrefu," alisema Saadah. Aliwataja mabondia wengine watakaopigana siku hiyo ni Emmanuel Mwakyembe dhidi ya Francis Miyeyusho, Mbaraka Mtange vs Hamza Mchanjo, Mwinyi Mzengela vs Ajemi Amani, Abdul Kubila vs Msabaha Salum, Omary Baraka vs Mukhsin Kizota, Ahmady Pelembela vs Idd Pazi na Florah Malechela atapambana na Halima Bandola.

## Serikali kuwapa mikopo wasanii

**Na ShufaaLyimo**

SERIKALI inatarajia kutoa mikopo ya sh. bilioni 1 kwa wasanii mbalimbali wa hapa nchini, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Hassan Abbas, alisema mikopo hiyo ni ya awamu ya pili na itatolewa leo kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Mwalimu Nyerere jijini, Dar es Salaam.

Abbas alisema wasanii watakaopata mikopo hiyo ni wale ambao watabainika kwamba wamekidhi vigezo vilivyowekwa na watatakiwa kukamilisha marejesho yake ndani ya miaka miwili.

Katibu huyo alisema mbali na kutoa mikopo hiyo ili kuwasaidia kujiendeleza, vilevile wanatarajia kulipokea vazi la Taifa ambalo litaonyesha uhalisia wa Mtanzania.

"Baada ya majadiliano ya muda mrefu kesho (leo) tunatarajia kulipokea vazi la Taifa ambalo lilitolewa mapendekezo na wadau mbalimbali," alisema Abbas.

## Mlandege yasaka kocha wa ubingwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABOSI wa Mlandege FC wamesema bado wanaendelea na mchakato wa kupata kocha mpya atakayerithi mikoba iliyoachwa na Mohamed Abdallah 'Bares' ambaye amejiunga na Tanzania Prisons inayoshiriki Ligi Kuu Bara.

Mwenyekiti wa Mlandege FC, Mbaraka Himid, aliliambia gazeti hili wanahitaji kupata kocha mpya mwenye uzoefu na atakayewasaidia kufikia malengo waliyoyaweka na si kurudi nyuma.

"Tunafanya mchakato huu kwa umakini, tunashirikiana kwa karibu ili tupate kocha ambaye ataendeleleza mafanikio yaliyopatikana katika msimu huu," alisema Himid.

Aliongeza wanajivunia mafanikio ambayo wameyapata tangu kuanza kwa msimu huu ambapo Bares aliiongoza vyema Mlandege na malengo yako makubwa ni kuendelea kufanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar baada ya kunyakua ubingwa wa Kombe la Mapinduzi.

Alisema wanafahamu mzunguko wa lala salama huwa na ushindani na changamoto mbalimbali, hivyo watahakikisha wanaajiri kocha atakayesaidia kupata mafanikio wanayoyatarajia.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**AYEW ATAKIWA EVERTON**

KLABU ya Everton inataka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ghana, Andre Ayew, ambaye anatarajiwa kuwasili England kwa mazungumzo ya uhamisho wa bure. Nottingham Forest pia inaweza kujaribu kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33. ***(Mail)***

**ISCO ANUKIA EVERTON**

EVERTON inaweza kufanya mchakato wa kumsajili kiungo wa kati wa zamani wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Isco mwenye umri wa miaka 30, ambaye anapatikana kwa uhamisho wa bure. ***(Times)***

**ZAPATA KUBAKIA ATALANTA**

KLABU ya Everton ilishindwa kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, Duvan Zapata, mwenye umri wa miaka 31 baada ya ombi lao kukataliwa na Atalanta. ***(TeamTalk)***

**CHILWELL ATAJWA CITY**

MLINZI wa Chelsea na England, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 26 ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na Manchester City msimu huu wa joto ikiwa mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Cancelo (28) atakosekana. ***(Times)***

**POTTER KUPEWA MUDA**

WAMIIKI wa Chelsea hawatadai matokeo ya haraka kutoka kwa Kocha, Graham Potter, kufuatia matumizi makubwa ya fedha waliyofanya katika usajili wa Januari. ***(Guardian)***

**MORGAN SOKONI EPL**

CHELSEA inatazamiwa kuongeza usajili mwingine katika safu ya ushambuliaji wakimtaka Jimmy-Jay Morgan mwenye umri wa miaka 17 ambaye atajiunga nao akitokea Southampton. ***(Sun)***

**UJUMBE WAMSAIDIA ZIYECH**

WINGA wa Chelsea kutoka Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29, alituma ujumbe mfupi wa maandishi kwa mmiliki wa klabu hiyo,Todd Boehly alipokuwa akijaribu kukamilisha uhamisho wake wa mkopo kwenda Paris St-Germain. ***(Mirror)***

**LEEDS YAMKATAA TUANZEBE**

LEEDS United ilikataa nafasi ya kumsajili beki, Axel Tuanzebe mwenye umri wa miaka 25 kwa mkopo kutoka Manchester United kabla ya dirisha la Januari kufungwa. ***(The Athletic, kupitia Metro)***

**FIRMINO HANA PRESHA**

WAKALA wa mshambuliaji wa Liverpool na Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 31 anaamini mazungumzo kuhusu kupewa mkataba mpya katika klabu hiyo yatakamilika mwezi huu. ***(Sky Germany)***

**CITY, BARCELONA VITANI**

KLABU ya Manchester City itapambana na Barcelona katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa Girona na Timu ya Taifa ya Hispania, mwenye umri wa chini ya miaka 21, Arnau Martinez. ***(Mundo Deportivo)***

**GIL ANUKIA SEVILLA**

SEVILLA ipo kwenye mazungumzo ya juu ya kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 21 kutoka Tottenham Hotspur kwa mkopo hadi mwisho wa msimu. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# PSG YAMALIZA HOFU KUKOSEKANA MBAPPE

●●●Kocha wake asema si jeraha baya sana kama ilivyotarajiwa huku...

**PARIS, Ufaransa**

JERAHA la Kylian Mbappe "halionekani kuwa mbaya sana", Kocha Mkuu wa Paris Saint-Germain, Christophe Galtier, amefichua baada ya mshambuliaji huyo kuchechemea walipokuwa wakicheza dhidi ya Montpellier.

Huku Neymar akiwa tayari ameondolewa katika mechi ya Ligue 1 kwa sababu ya uchovu wa misuli, Mbappe alilazimika kutolewa nje dakika ya 21 kwenye mechi ya ushindi wa mabao 3-1 kutokana na kushika msuli wake wa paja alipokuwa akiondoka uwanjani.

Jeraha la fowadi huyo lilikuja baada ya kukosa penalti ingawa

kupitia mabao ya Lionel Messi, Fabian Ruiz na Warren Zaire-Emery mwenye umri wa miaka 16.

Lakini baada ya Sergio Ramos pia kutoka na jeraha katika kipindi cha kwanza, kulikuwa na wasiwasi mkubwa baada ya mchezo juu ya upatikanaji wa wachezaji chini ya wiki mbili hadi mechi ya kwanza ya PSG ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich.

Galtier alipunguza hofu juu ya majeraha ya Mbappe na Ramos, ingawa, aliwaambia waandishi wa habari kwenye mkutano wake baada ya mechi: "Haionekani kuwa mbaya sana, kwa mmoja kama kwa mwingine.

wawili muhimu. Juu ya kile tulichoona wakati wa mapumziko na kile tulichoambiana, hakuna wasiwasi sana."

Licha ya PSG kushinda Ligue 1 msimu uliopita, Kocha Mkuu, Mauricio Pochettino, aliachishwa kazi baada ya kushindwa kutwaa taji la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Galtier anajinadi ili kuepuka hatima hiyo hiyo, ingawa amesema alitarajia shinikizo kabla hajaingia kazini. "Ndiyo, moja kwa moja unaposaini PSG, kuna wajibu wa kushinda," alisema.

"Ligi ya Mabingwa Ulaya inakuhitaji uwe tayari. Tuna wachezaji wanaorejea, na tumekuwa na Kombe la Dunia. Nilijua kabla ya kuja kuli-

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,072,5
MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
SINGIDA BS FC
1 | 1.15
X | 4.00
2 | 7.28
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# XAVI AMFANANISHA PEDRI NA INIESTA

**BARCELONA, Hispania**

XAVI alimtaja Pedri kwa sifa baada ya Barcelona kuendelea kukaa kileleni mwa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa pointi nane baada ya kuwafunga Real Betis, akimlinganisha kiungo huyo na "kipaji bora" wa Hispania, Andres Iniesta.

Mabao kutoka kwa Raphinha na Robert Lewandowski yaliimarisha jitihada za Barca kutwaa ubingwa waliposhinda 2-1 kwenye Uwanja wa Benito Villamarin hapo juzi.

Akizungumza baada ya Barca kuongeza shinikizo zaidi kwa wapinzani wao wa taji Real Madrid, ambao walitarajia kuwakaribisha Valencia jana, Xavi alimmwagia sifa kiungo huyo duni.

"Ni mchezaji ambaye yuko kwenye kiwango kingine, nimeona wachache sana kama yeye," alisema Xavi.

"Andres ndiye kipaji kikubwa zaidi ambacho nimewahi kuona katika soka la Hispania, lakini Pedri anafanana naye sana. Anaweza kuleta mabadiliko, na tayari anafanya hivyo."

Pedri hakuwa mchezaji pekee mchanga aliyeng'ara kwa Barca, kwani Alejandro Balde aliandikisha pasi yake ya nne msimu huu na kumuwezesha Raphinha kufunga.

# Sancho, Martial kuibeba United

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag anatumaini Manchester United itaendelea kuwa kamili kwenye safu ya ushambuliaji baada ya kurejea kwa Jadon Sancho na Antony Martial.

Washambuliaji hao wawili walikuwa wachezaji wa akiba kipindi cha pili katika ushindi wa mabao 2-0 wa mechi ya nusu fainali ya Kombe la Carabao iliyochezwa dhidi ya Nottingham Forest kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi usiku.

Kurejea kwa wawili hao ni muungano mzuri pamoja na uwepo wa Marcus Rashford, Antony, Bruno Fernandes na Wout Weghorst.

"Natumaini tutafika mahali wanapopatikana wote, ukitaka kushinda mataji wanatakiwa kuwepo kwa sababu tuna michezo mingi.

"Uliona leo (juzi), unaweza kufanya kitu kutoka kwenye benchi, kuleta nguvu tofauti."

Mabadiliko mara tatu ya United kwenye alama ya saa yalisababisha ushindi dhidi ya Forest, huku Sancho akiwa miongoni mwao katika mechi yake ya kwanza kuichezea klabu hiyo tangu Oktoba.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alicheza nafasi tofauti na ilivyotarajiwa, akichukua nafasi ya kati zaidi ya moja kwenye winga, na uwezo wa aina mbalimbali kitu ambacho Ten Hag anataka kukitumia.



## HABARI MICHEZO


549,524/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/02/23 | 18:00 | Preston North End vs Bristol City | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 02. 04/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Queens Park Rangers | 3.00 | 3.20 | 2.39 |
| 03. 04/02/23 | 18:00 | Reading FC vs Watford FC | 2.70 | 3.20 | 2.60 |
| 04. 04/02/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KVC Westerlo | 2.75 | 3.45 | 2.41 |
| 05. 04/02/23 | 22:00 | FC Emmen vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 04/02/23 | 23:00 | Excelsior Rotterdam vs RKC Waalwijk | 2.70 | 3.35 | 2.49 |
| 07. 04/02/23 | 23:00 | Stade Rennes vs Lille OSC | 2.30 | 3.35 | 2.95 |
| 08. 04/02/23 | 23:30 | Estoril Praia vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 09. 05/02/23 | 03:30 | Atletico Lanus vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.31 | 2.85 | 2.80 |
| 10. 05/02/23 | 03:30 | Argentinos Juniors vs Racing Club Avellaneda | 2.60 | 2.70 | 2.60 |
| 11. 05/02/23 | 15:30 | Royal Antwerp FC vs Club Brugge | 2.49 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 05/02/23 | 16:00 | Villarreal CF B vs Granada CF | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 13. 05/02/23 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.49 | 3.15 | 2.37 |
| 14. 05/02/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs NEC Nijmegen | 2.40 | 3.35 | 2.85 |
| 15. 05/02/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Leeds United | 2.60 | 3.30 | 2.60 |
| 16. 05/02/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs FC Nantes | 2.65 | 3.10 | 2.70 |
| 17. 05/02/23 | 17:00 | Torino FC vs Udinese Calcio | 2.24 | 3.20 | 3.25 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 03/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3373 | Tiddim Road Athletic Club vs Mohammedan SC | 2.50 | 3.21 | 2.57 |
| 14:00 | 4321 | Port FC vs BEC Tero Sasana | 1.56 | 3.85 | 5.00 |
| 15:15 | 2117 | Al Hikma vs Salam Zgharta | 1.75 | 3.22 | 4.57 |
| 16:00 | 1133 | Tanzania Prisons vs Mtibwa Sugar | 2.16 | 2.84 | 3.51 |
| 16:00 | 1227 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Acre | 2.31 | 3.04 | 3.25 |
| 16:00 | 2570 | Rukinzo FC vs TOP Junior FC | 1.93 | 3.11 | 3.84 |
| 16:00 | 3081 | Maccabi Jaffa vs Bnei Yehuda | 2.81 | 3.13 | 2.53 |
| 16:00 | 5241 | Gorilla FC vs Gasogi United | 2.70 | 2.60 | 2.55 |
| 16:00 | 5306 | Hapoel Ramat Gan vs Ahi Nazareth | 2.88 | 3.20 | 2.43 |
| 16:00 | 5411 | Hapoel Rishon Lezion vs Ironi Hasharon | 2.10 | 3.10 | 3.68 |
| 16:20 | 5136 | Fursan Hispania FC vs Dubba Al-Husun | 14.53 | 6.44 | 1.14 |
| 18:00 | 5016 | Chindia Targoviste vs UTA Arad | 2.55 | 3.04 | 2.78 |
| 18:30 | 5997 | Pafos FC vs Nea Salamis | 1.50 | 4.05 | 6.39 |
| 19:00 | 3408 | Simba vs Singida BS FC | 1.15 | 4.00 | 7.28 |
| 19:00 | 3753 | Moroka Swallows FC vs Richards Bay FC | 2.86 | 2.86 | 2.63 |
| 19:00 | 5070 | Istra vs Vsnk Varazdin | 2.19 | 3.10 | 3.10 |
| 20:00 | 2025 | Altay vs Adanaspor | 2.31 | 3.16 | 2.85 |
| 20:00 | 3168 | Wolfsberger AC vs Rapid Vienna | 2.80 | 3.53 | 2.18 |
| 20:00 | 4922 | Wisla Plock vs Warta Poznan | 2.20 | 3.05 | 3.15 |
| 20:30 | 2169 | Paderborn vs Fortuna Dusseldorf | 2.20 | 3.46 | 2.97 |
| 20:30 | 2226 | Sandhausen vs SV Darmstadt | 3.66 | 3.46 | 1.93 |
| 20:30 | 3781 | Maritzburg Utd vs Amazulu | 2.60 | 2.85 | 2.90 |
| 21:00 | 1195 | U Craiova SA vs Universitatea Cluj | 2.16 | 3.12 | 3.38 |
| 21:00 | 2390 | Apoel Nicosia vs Apollon Limassol | 1.85 | 3.41 | 4.21 |
| 21:30 | 1728 | Dunkerque vs Nancy | 2.40 | 3.04 | 2.94 |
| 21:30 | 3453 | Red Star vs Sedan | 1.74 | 3.57 | 4.31 |
| 22:00 | 1959 | Niger vs Madagascar | 3.10 | 3.00 | 2.41 |
| 22:00 | 2330 | Willem II Tilburg vs Helmond Sport | 1.50 | 4.05 | 5.90 |
| 22:00 | 2772 | Dordrecht vs FC Eindhoven | 3.37 | 3.42 | 2.02 |
| 22:00 | 3067 | ADO Den Haag vs NAC Breda | 1.99 | 3.52 | 3.36 |
| 22:00 | 3619 | Jong AZ Alkmaar vs VVV Venlo | 2.57 | 3.42 | 2.48 |
| 22:00 | 4412 | Puskas Akademia vs Vasas SC | 1.58 | 3.68 | 5.08 |
| 22:00 | 5043 | De Graafschap vs Telstar | 1.74 | 3.67 | 4.20 |
| 22:00 | 5106 | Almere City vs Jong PSV | 1.74 | 3.68 | 4.21 |
| 22:00 | 5135 | Heracles Almelo vs Jong Utrecht | 1.37 | 4.82 | 6.71 |
| 22:00 | 5236 | Fortuna Sittard vs Sparta Rotterdam | 2.68 | 3.28 | 2.48 |
| 22:00 | 5645 | FC Oss vs Den Bosch | 2.43 | 3.32 | 2.69 |
| 22:30 | 1640 | Widzew Lodz vs Jagiellonia | 1.98 | 3.26 | 3.47 |
| 22:30 | 2180 | Augsburg vs Bayer Leverkusen | 3.97 | 3.82 | 1.77 |
| 22:30 | 3188 | Modena vs Cagliari | 2.55 | 3.16 | 2.69 |
| 22:45 | 1327 | PAU FC vs Bordeaux | 3.57 | 3.17 | 2.06 |
| 22:45 | 2721 | Dijon vs Niort | 1.87 | 3.33 | 4.08 |
| 22:45 | 3878 | Rodez Aveyron vs Sochaux | 3.22 | 3.07 | 2.26 |
| 22:45 | 4535 | Oostende vs Anderlecht | 3.49 | 3.59 | 1.96 |
| 22:45 | 4981 | Queens Park vs Ayr United | 2.03 | 3.56 | 3.20 |
| 23:00 | 2588 | Malaga vs Real Oviedo | 2.39 | 2.82 | 3.27 |
| 23:00 | 3818 | Chelsea vs Fulham | 1.59 | 3.88 | 5.17 |
| 23:00 | 5717 | West Bromwich vs Coventry | 1.75 | 3.51 | 4.45 |
| 23:00 | 5779 | Athletic Bilbao vs Cadiz CF | 1.41 | 4.30 | 7.80 |
| 23:15 | 1536 | Sporting Farense vs CF Estrela | 2.05 | 3.30 | 3.40 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# PHIRI AFUNGUKA ATAREJEA DIMBANI NA MAKALI YAKE

**Na Saada Akida**

KINARA wa mabao katika kikosi cha Simba, Moses Phiri, ametamba atarejea kivingine katika kuisaidia timu yake baada ya kupona majeraha yaliyokuwa yanamsumbua na ameahidi ataendelea kuwafurahisha mashabiki kwa kuzifumania nyavu.

Phiri alikuwa nje kwa muda mrefu kutokana na anatarajiwa kuonekana kwa mara ya kwanza katika mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Al Hilal, utakaopigwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Akizungumza na gazeti hili jana katika mazoezi ya Simba yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena uliopo Bunju, Phiri alisema ushindani wa namba umekuwa mkubwa baada ya kusajiliwa wachezaji wapya, hivyo analazimika kupambana ili kurudisha nafasi yake.

Mzambia huyo alisema anafuraha kurejea uwanjani ili kuendelea na mapambano ya kufanikisha wanafikia malengo ya msimu huu.

"Sio kitu kizuri kwa mchezaji kukosa mechi nyingi kutokana na majeruhi, lakini nimejipanga kuhakikisha narudi kwa nguvu kama nilivyoanza msimu," alisema Phiri.

Aliongeza kwa sasa yuko fiti baada ya kumalizika mchezo dhidi ya Singida Big Stars atakuwa tayari kucheza endapo atapangwa.

"Nimejipanga kuendelea pale nilipoishia, ninataka kuonyesha ubora wangu," Phiri alisema.

Kuhusu ujio wa mshambuliaji, Jean Baleke, Phiri alisema mchezaji huyo ni mzuri, ana kasi na pia anajua kufunga .

"Baleke yuko vizuri ninaimani atai-saidia timu, kwa kushirikiana naye tutafikia malengo tuliojiwekea katika timu yetu," alisema Phiri.




# SIMBA, SINGIDA BS

INATOKA UK. 24

hamu ya juu kuhakikisha wanafanikiwa malengo yao ya kutafuta pointi tatu muhimu.

Pluijm alisema watacheza mchezo huo kwa ufundi na umakini kwa sababu ya ukubwa na ubora wa wapinzani wao ambao hivi karibuni wamepata kocha mpya ambaye amechangia kuiboresha timu.

"Hii ni mechi ngumu na yenye ushindani mkubwa kwa sababu Simba ni timu kubwa na wachezaji wake ni wazuri, tunafahamu ubora wao na vijana wangu wako tayari kwa ajili ya mchezo wetu na kurejea nyumbani na pointi muhimu.

Tumejiandaa vizuri kuwakabili Simba najua wanahitaji kupata ushindi lakini hatuwezi kuwa daraja lao la kuongeza alama na kupanda katika msimamo wa ligi, hatupo tayari kuruhusu hilo," alisema Pluijm.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Tanzania Prisons dhidi ya Mtibwa Sugar wakati kesho Yanga itaikaribisha Namungo FC kutoka Lindi, Coastal Union itaifuata Geita Gold huku Dodoma Jiji wakiwakaribisha Azam FC kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo, amesema mchakato wa kupata kocha mpya wa kuinoa Timu ya Taifa (Taifa Stars), uko katika hatua za mwisho lakini watazingatia mwalimu anayefahamu vyema soka la Afrika.

# SPORTPESA YAIPA YANGA SIKU TATU

INATOKA UK. 24

tumemaliza tutakuja kukiweka hadharani," alisema Hersi.

Hata hivyo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, hakupatikana kuthibitisha kupelekwa kwa barua hiyo au kusema lolote kuhusiana na sakata la mkataba linaloendelea kati ya Yanga na SportPesa.

Kwa sasa kikosi cha Yanga kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuikaribisha Namungo FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Michezo
Ijumaa Februari 3, 2023
Nipashe



PSG yamaliza hofu kukosekana Mbappe

UKURASA 21

# SIMBA, SINGIDA BS VITA YA WAKONGWE

## ●●●Makocha watamba kukamilisha hesabu, Kocha mpya Stars anukia...

**Na Saada Akida**

VITA ya kujiimarisha kileleni inatarajia kuendelea kwa Simba maarufu Wekundu wa Msimbazi kuikaribisha Singida Big Stars FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Timu hizo zitashuka dimbani zikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare katika mechi ya mzunguko wa kazi iliyofanyika kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida.

Katika mechi ya leo, Simba itaendelea kumkosa mshambuliaji wake, Moses Phiri, ambaye kwa sasa anafanya programu maalum kwa ajili ya kujiimarisha wakati Singida Big Stars watamkosa, Deus Kaseke aliyefungiwa mechi tatu na Kamati ya Uendeshaji ya Ligi kutokana na kubainika kufanya vitendo cha ushirikina.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' alisema mchezo huo utakuwa mgumu na timu yake imejipanga kufanya kila kitu ili kuhakikisha wanapata ushindi na si matokeo mengine.

Robertinho alisema kikosi chake kinahitaji ushindi na anaamini matokeo chanya yatasaidia kuongeza morali kuelekea mchezo ujao wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC utakaochezwa ugenini, huko Guinea.

"Tumejiandaa vizuri na wachezaji wangu wako tayari kupambana kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huu ili kuendelea kujiweka katika mazingira mazuri ya kuwania ubingw, ushindi utatuongezea molari kuelekea mchezo wetu wa Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Robertinho.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo dhidi ya Singida Big Stars yanaendelea vizuri na kila mchezaji anafahamu ugumu wa ratiba za michezo waliyonayo katika mwezi huu.

Zimbwe Jr alisema kwao kila mechi ni sawa na fainali, hivyo watapambana katika kiwango cha juu ili kupata ushindi na kujiimarisha kwenye mbio za kuwania ubingwa wa ligi.

"Mchezo wa kwanza dhidi ya Singida Big Stars uliisha kwa sare, kuna mapungufu yaliyojitokeza ambayo tumeyafanyia kazi mazoezini na mazuri tutayaendeleza, kitu kizuri mwalimu amerudi. Kikubwa tunawaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi tunawahitaji sana kipindi hiki kwa ajili ya kuongeza hamasa," alisema Zimbwe Jr.

Naye Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, alisema wamejiandaa vizuri na watashuka dimbani kwa nid-

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri akijifua baada ya kupona majeruhi. **PICHA: SIMBA SC**

## SportPesa yaipa Yanga siku tatu

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanadaiwa kupewa siku tatu na Kampuni ya Kubashiri Michezo ya SportPesa kuondoa neno Haier kwenye jezi zao mpya walizozindua hivi karibuni, imefahamika.

Mapema wiki hii Yanga iliingia mkataba na Kampuni ya Haier kwa ajili ya mechi zao za kimataifa za mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika wenye thamani ya Sh. bilioni 1.5.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zinasema SportPesa pia imepeleka nakala nyingine ya barua katika Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ikielezea masikitiko yao dhidi ya Yanga na hatua ambazo wanahitaji zichukuliwe kwa sasa.

Chanzo hicho kiliendelea kusema mabosi wa SportPesa wameendelea na msimamo wao kwa kuwataka Yanga kuachana na mdhamini wao mpya kwa sababu wanakiuka makubaliano ya mkataba ambao waliingia nao mwaka jana.

"Nakala ya barua imepelekwa TFF kwa sababu ni msimamizi wa timu zote zinazoshiriki Ligi za hapa Tanzania ikiwamo Yanga ambao ni mtoto wa shirikisho hilo.

"Kampuni hiyo imewapa Yanga siku tatu kuhakikisha wametekeleza agizo hilo kabla ya hatua zaidi za kisheria hazijachukuliwa," kilisema chanzo chetu.

Rais wa Yanga, Hersi Said, aliliambia gazeti hili bado klabu yao na SportPesa wanaendelea na majadiliano kwa ajili ya kulimaliza sakata hilo lililojitokeza baina ya pande hizo mbili.

Hersi alisema wanafahamu vyema Sportpesa ndio wadhamini wao wakuu na wanafuata na kuheshimu taratibu zote za kimkataba zilizokuwepo.

"Mazungumzo yetu yalikuwa wazi katika kusaini mkataba na Haier, hatuwezi kuitumia SportPesa katika michuano ya CAF, Yanga iliona inaweza kutafuta mdhamini mwingine wa muda. Tuna mawasiliano yote wakati tunafanya nao (majadiliano), lakini sio vyema kuweka kila kitu hadharani, taratibu za kiutendaji zinakwenda vyema na tutakapokuwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002